SUPA JACKPOT
TZS. 1,112,462,859
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Rasmi** shtaka la mkulima dhidi ya mawaziri, vigogo aliowataja CAG

UKURASA 3


BUFE
IJUMAA MEI 12, 2023 Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Mikopo halmashauri inavyogeuka mzigo mabilioni serikalini, badala mtaji wa umma
UCHUMI
Alichowekeza Samia Royal Tour, yajibu kwa watalii Hifadhi Katavi
• Rasmi, aliyoyatamka kwenye uzinduzi...

UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Mei 12, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581308

www.ippmedia.com

...lian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# KASHFA NZITO

• **Askari**-pori wadaiwa kuwavua nguo, kuwachoma moto wafugaji, waua mifugo kwa risasi.
• **Majaliwa** atoa saa 24... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO



UKURASA WA 8
**BOSI MICROSOFT APONGEZA JITIHADA ZA RAIS SAMIA**
MTENDAJI Mkuu wa Masuala ya Teknolojia wa Kampuni ya...

UKURASA WA 19
**CHADEMA YAFAFANUA KAULI YA LISSU KUHUSU MARIDHIANO**
MKURUGENZI wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo...




Wanachama wa Baraza la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), wakiandamana kutoka Posta ya zamani hadi Ofisi ndogo za Bunge jijini Dar es Salaam jana, kumshinikiza Spika wa Bunge, kuwaondoa bungeni wabunge 19 wa viti maalum waliofutwa uanachama na chama hicho. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Aweso: tunayatoa maji ziwani hadi penye uhaba zaidi

**BIL. 756/-**

1. Kila wilaya kujengewa bwawa la kuvuna maji ya mvua
2. Vyanzo vya maji 84 kutangazwa kuwa maeneo tengefu
3. Ujenzi wa Bwawa la Kidunda na Farkwa kutiliwa mkazo

UKURASA 4,11,12&13

# Posho saa za ziada kurudi kwa watumishi serikalini

UK.2

MICHEZO SIMBA YAITANGAZIA 'UBAYA' RUVU BARA UK.24

KATUNI UK.6



Waziri Mkuu, Kasimu Mjaliwa akijibu maswali ya yaliyoulizwa na baadhi ya Wabunge kwenye kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu katika mkutano wa 11 kikao cha 23 cha Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge aibua madai askari wa TANAPA kudhalilisha wananchi

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Mbarali (CCM), Francis Mtega, ameibua bungeni madai kwamba wananchi wa kijiji cha Mwanadhali, Mbarali mkoani Mbeya, kwamba wamefanyiwa vitendo vya ukatili, udhalilishaji na maofisa wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Katika madai hayo, amesema kinamama wa kijiji hicho walivuliwa nguo na kubaki watupu kisha kuunguzwa mwilini na panga lenye moto, huku vijana wakipigwa na wafugaji kuporwa mifugo.

Mbunge huyo alieleza hayo jana baada ya kipindi cha maswali na majibu, akimwomba Spika wa Bunge Dk. Tulia Ackson, kusitisha shughuli za Bunge na wabunge waanze kujadili suala hilo la dharura

Akisimulia mkasa huo, mbunge huyo alisema Mei 6, mwaka huu, ilifika helkopta katika kijiji hicho iliyokuwa na watumishi wa TANAPA na kuwavamia wananchi, kuwapiga, kuwavua nguo kinamama, kupora zaidi ya mifugo 250 ya mfugaji.

Kwa mujibu wa mbunge huyo, mmiliki wa mifugo hiyo alisalimu amri na kuachia mifugo yake kuporwa na maofisa hao, hali iliyomsababisha kuathirika kisaikolojia na kutaka kujiua.

Akisimulia zaidi, Mtega alisema kuna kijana mwingine aliyekuwa akipinga kuporwa mifugo yake lakini aliambulia kipigo kutoka kwa maofisa hao hali iliyomlazimu kulazwa hospitalini.

"Yule aliyeporwa mifugo hivi sasa wananchi wanafanya kazi ya kumfariji ili asitimize kusudio lake la kujiua. Huyo kijana aliyelazwa hospitalini ninazo picha zake namna alivyoumizwa. Nikizionyesha hapa kwenye televisheni (bungeni) nina hakika wabunge wote mtatokwa na machozi," alisema Mtega.

**KUVULIWA NGUO**

Mtega alisema maofisa hao mbali na kutekeleza kitendo hicho waliwavua nguo kinamama na kubaki watupu kisha wakachukua panga wakaweka kwenye moto na kuwababua miili yao.

"Wale wananchi wanamshukuru rubani wa ile helkopta aliona huruma, aliingilia kati na kuwaomba wale maofisa wasiwaue," alisema.

Mtega alisema baada ya kusitisha vitendo hivyo, maofisa hao waliwapiga risasi mbuzi wawili na mbwa watatu kisha wakaondoka.

"Vitendo hivi kama serikali haitachukua hatua za haraka, vinaleta taharuki kubwa. Viongozi wangu wa CCM waliumia sana wakiwamo madiwani wanaumiza vichwa, hawana cha kuwaambia wananchi. Hili limechonganisha wananchi na serikali yao. Kwa kweli hali ni mbaya sana Mbarali.

"Ninaomba kutoa hoja ya kuahirisha mjadala unaoendelea sasa ili kujadili jambo hili la dharura linaloendelea jimboni kwangu naomba kutoa hoja Mh.Spika" alisema.

**MAAGIZO YA PM**

Baada ya kueleza hayo, Spika Tulia alimpa nafasi Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kutoa majibu ya serikali na kusema: "Serikali imemsikia mbunge akizungumzia matatizo ambayo serikali ilishatoa maelekezo ilipofanya ziara kwenye eneo hilo.

"Kwanza nimsihi asisitishe shughuli za Bunge, niwaombe pia wabunge msimuunge mkono. Nawaomba hivyo kwa kuwa jambo hili ni nyeti na najua lina tatizo.

"Naiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii sasa hivi popote walipo, Waziri, Katibu Mkuu na Mtendaji Mkuu wa TANAPA waende mkoani Mbeya kukutana na Mkuu wa Mkoa kwa kuwa tulipokuwa Mbarali na kutoa maelekezo ya vijiji vyote vilivyokuwa na mgogoro wa GN 28 kulikuwa na vijiji zaidi ya 32. Baada ya mapitio kuona yale maeneo kama je yana tija kwa wakulima au kwa hifadhi tuliridhika kwamba vijijini 27 havina tija."

Alisema waliviruhusu vijiji hivyo viachwe, wananchi waendelee na kilimo na kwamba vijiji vitano vilivyokuwa kwenye eneo oevu ilikubaliwa kwamba wawakilishi wa wilaya, viongozi wa mkoa na TANAPA viachwe kwa muda huu kwa sababu tayari wananchi walishaanza maandalizi ya kilimo, kwamba waendelee na kilimo mpaka mazao yatakapoiva.

Baada ya serikali kukamilisha tathmini katika vijiji hivyo, alisema wananchi wataambiwa waondoke waende kwenye maeneo ambayo wameelekezwa na watakuwa wameshalipwa fidia yao.

Majaliwa alisema vijiji vitatu wananchi wake walitakiwa kuondoka kwa kuwa viko kwenye eneo oevu.

"Maelekezo haya tuliyatoa, tulikutana na wananchi kwenye mkutano wa hadhara, wananchi walifurahi lakini najua ni tofauti kwa wale walioambiwa waondoke moja kwa moja vijiji vitatu. Lakini vijiji 27 viliruhusiwa vibaki kwenye maeneo yao.

"Suala hili la mbunge namuahidi serikali inakwenda kuchukua hatua mara moja ya kwenda kwa kumuagiza waziri na timu yake ya wizara pamoja na Mtendaji Mkuu wa TANAPA waende eneo hilo," alisisitiza.

Alisema maofisa wanaotuhumiwa kufanya vitendo hivyo hawakupaswa kufanya hivyo pasipo kumshirikisha wakuu wa wilaya na mkoa ambao wanajua agizo, hivyo serikali itafuatilia suala hilo na kuchukua hatua muhimu.

**KAULI YA SPIKA**

Baada ya Majaliwa kutoa maelezo hayo, Spika Tulia alisema: "Natarajia kwamba hawa watu wataenda huko leo (jana)."

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
07 - 10 - 2022

TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumamosi tarehe 13-05-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili:

**T 483 ECF / T 630 AJA**
**T 967 DTN / T 273 DUH**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 26.00   Upana - mita 4.20   Kimo - mita 4.80**

3. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi, gari itasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

# Posho saa za ziada kurudi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI iko katika maandalizi ya mwongozo wa ulipaji posho ya saa za ziada zilizofutwa mwaka 2014, ikisisitiza haina posho ya mazingira magumu kwa walimu.

Kifungu cha 7(3) cha Sheria ya Mapato ya Mwaka 2014 kiliondoa posho za nyumba, usafiri, madaraka, kufanya kazi saa za ziada, kufanya kazi katika mazingira magumu na honoraria kwa mtumishi wa serikali au taasisi ambayo bajeti yake hulipwa yote au kwa kiwango kikubwa na ruzuku za serikali.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratias Ndejembi, aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Kunti Majala.

Mbunge huyo alitaka kujua lini serikali itatoa posho ya mazingira magumu kwa walimu walioko vijijini, hususani walimu wanawake.

Naibu Waziri huyo alisema serikali inaweka uwezeshaji kwa walimu kwa kujenga nyumba karibu na shule. Hakuna posho mahususi ya mazingira magumu inayotolewa na kwa sasa. Wanaendelea na kazi ya kuandaa mwongozo wa ulipaji posho kwa saa za ziada.

Awali wakati wa kipindi cha 'Maswali kwa Waziri Mkuu', Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Kassim Majaliwa alitaja mikakati mbalimbali ya serikali kuitumia Siku ya Familia Mei 15 kutoa elimu na kukemea mmonyoko wa maadili kwa jamii.

Majaliwa, akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Aysharose Mattembe, alisema kuna tatizo la mmonyoko wa maadili na serikali ipo mstari wa mbele kukemea na Tanzania inasherehekea siku hiyo kwa kukutana na kutoa elimu kwa umma kuhakikisha maadili ya nchi yanazingatiwa ili kuwa na kizazi endelevu.

Aliagiza wakuu wa mikoa na wilaya chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kujipanga kutumia siku hiyo kutoa elimu na kukemea ukiukwaji wa maadili ili kulinda taifa kwa kuwa na maadili mema. Majaliwa pia alitoa ufafanuzi kuhusu uhusiano wa Tanzania na Denmark, akilihakikishia Bunge kuwa Tanzania ni nchi salama na ina uhusiano mzuri na nchi hiyo kidiplomasia, kisiasa na kiuchumi.

Kutokana na nchi hiyo kukusudia kubadilisha sera za nchi za nje mwaka 2024 inayolenga kufungua balozi kwenye nchi zisizo salama, Majaliwa alisema kuwa kwa sasa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia viongozi wakuu wa nchi hizo, wapo katika mazungumzo ili kubadilisha mwelekeo huo.

Waziri Mkuu alitoa ufafanuzi huo baada ya Mbunge wa Chakechake, Ramadhan Suleiman Ramadhan, kutaka kujua kauli ya serikali kuhusiana na kuwapo taarifa ya baadhi ya balozi kutangaza kufunga ofisi zake nchini, ukiwamo Ubalozi wa Denmark.

**HABARI KITAIFA**

# Rasmi mkulima kuwashtaki mawaziri waliotajwa na CAG

**Na Grace Gurisha**

MKULIMA Thomas Nkola ametamka kuwasilisha rasmi maombi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akiomba kufungua mashauri tisa dhidi ya mawaziri, wakuu wa taasisi na kampuni binafsi waliohusishwa na ubadhirifu wa fedha za umma, wakiitia serikali hasara ya Sh. trilioni 8.4.

Ni shauri ambalo msingi wake unatokana na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya Mwaka 2022/23, ikiwahusisha wadaiwa hao dhidi ya hasara ya kiasi tajwa cha fedha.

Katika madai yake, mkulima huyo ameelekeza malalamiko ya ubadhirifu maalum unaohusu ukopaji wa fedha nyingi za umma, pia hasara za jumla zikigusa mamlaka kuu za kiserikali zikiwamo dola, hali kadhalika wadau binafsi - washirika wa maendeleo na kampuni kubwa ya kimataifa inayofanya kazi nchini.

Nje ya viwanja vya mahakama hiyo jana, mkulima huyo alidai aliwasilisha malalamiko hayo ya kisheria dhidi ya mawazi; Dk. Mwigulu Nchemba (Fedha na Mipango), January Makamba (Nishati) na Prof. Makame Mbarawa (Ujenzi na Uchukuzi).

Wengine katika orodha hiyo ni Prof. Palamagamba Kabudi ambaye ana jukumu maalum katika mikataba ya serikali, Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Vilevile, amewajumuisha Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli (TRC), Masanja Kadogosa, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutupa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme (TANESCO), Maharage Chande.

Pia wamo; Erdem Arioglu, Makamu Mwenyekiti wa Kampuni ya Yapi Merkez inayojenga reliya kisasa (SGR). Hati ya maombi pia ina majina ya Rogatus Mativilaz kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Japhet Justine na Habinder Sigh Seth, ambao hawajatajwa nafasi zao wala taasisi wanazotoka.

Wakili wa mkulima huyo, Penina Ernest alidai mteja wake amefungua kesi hizo chini ya Ibara ya 27 (1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tayari kesi tano zimefunguliwa.

Alizitaja kesi hizo ni namba 13, 14, 15,16 na 17 za mwaka 2023, ambazo zimepangwa kwa mahakimu wakuu tofauti wa mahakama hiyo ambao ni Pamela Mazengo, Huruma Shaidi, Richard Kabate, Evodia Kyaruzi na Mary Mrio.

Alidai kuwa katika kesi zote, mteja wake anadai watu hao wamefanya ubadhirifu wa fedha za umma. Hatua za kisheria zichukuliwe. Ikiwezekana warudishe fedha hizo au wafilisiwe.

# Wanafunzi 2 walivyofariki ajali ya lori

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WANAFUNZI wawili wa Shule ya Sekondari ya Mpalanga, wilayani Bahi, mkoani Dodoma wamefariki na wengine zaidi ya 31 kujeruhiwa katika ajali ya lori lenye namba T519 DSY walilokuwa wamepanda, kupinduka wakati wakiwa safarini kwenda kwenye kambi ya michezo ya UMISETA.

Wakizungumza na waandishi wa habari baadhi ya majeruhi wa ajali hiyo waliolazwa katika hospitali ya Rufani ya mkoa wa Dodoma, walisema mwendokasi wa dereva ndiyo chanzo cha ajali hiyo.

Amani Yobwa, mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule hiyo, alisema walipanda usafiri huo kwenda kushiriki michezo ya UMISETA ambayo ilikuwa imepangwa kufanyika katika Kijiji cha Magaga.

"Tulipakiwa kwenye gari lile asubuhi ili kuwahi michezo ya Umiseta, lakini tulipofika katika kijiji cha Chidilo kuna eneo kuna kona kali dereva alipokata kona gari likapoteza mwelekeo na kupinduka na kusababisha wenzetu wawili kufa na sisi kujeruhiwa," alisema Yobwa.

Magreth Masinga, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika shule hiyo alisema sababu za ajali hiyo ni mwendokasi wa gari walilotumia ambalo sio kwa ajili ya abiria.

Mmoja wa wazazi wa wanafunzi waliopata ajali hiyo Manase Matonya, alisema wanaiomba serikali kwenye matukio mbalimbali ya wanafunzi kuacha kutumia magari ya mizigo kubeba abiria.

Aidha, taarifa iliyotolewa na uongozi wa Wilaya ya Bahi, ilisema ajali hiyo imetokea Kijiji cha Chidilo majira ya saa tano asubuhi, Kata ya Mpalanga, Tarafa ya Chipanga.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa gari ilikuwa aina ya canter ilikuwa imebeba jumla ya wanafunzi 46 wakitokea Mpalanga Sekondari kwenda Magaga Sekondari kwenye michezo hiyo.

"Wanafunzi wawili wa kike wamefariki dunia hapo hapo majina yao ni Neema Yohana Hoya (17) kidato cha tatu mkazi wa Chidilo na Magreth Juma (19), mkazi wa Nholi na wanafunzi 31 wamepelekwa Hospitali ya Rufani Dodoma kwa matibabu zaidi na wengine 14 wamepatiwa matibabu zahati ya Mpalanga," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Ernest Ibenzi, alithibitisha kupokea majeruhi 31 wanaoendelea kupata matibabu.

"Majira ya saa 7:30 tulipokea majeruhi hao wanafunzi na wanne kati yao wamefanyiwa upasuaji na wengine walikuwa na majeraha madogo wanaendelea vizuri," alisema Dk. Ibenzi.


**GARDAWORLD**
**KENYA KAZI SECURITY ( T ) LTD**

**INVITATION FOR BIDS**
**SALE OF ASSETS**
**TENDER No: GW/FY2023/01**
**BIDS TO REACH US ON OR BEFORE FRIDAY 19TH MAY 2023**

Bids are invited from interested parties for the purchase of assets as listed below:

| SNo: | REG NO: | MAKE | MODEL | CC | STATUS | LOCATION |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MC184AXB | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 2 | MC377AAQ | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 3 | MC920BXG | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 4 | XLAAHAKKC7H500020 | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 5 | MC689AAN | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 6 | MC862AGQ | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 7 | MC976AEM | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 8 | MC770ABY | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 9 | MC373CLW | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 10 | MC706ABY | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 11 | MC769ABY | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 12 | MC105AAU | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 13 | MC435BXL | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 14 | MC348BRJ | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 15 | MD21213Z00WL10503 | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 16 | MC774ABY | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 17 | MC762ABY | Motorcycle | | | grounded | DSM |
| 18 | MC106BXP | Motorcycle | | | Offroad | DSM |
| 19 | MC948BXN | Motorcycle | | | Offroad | DSM |
| 20 | MC257AAM | Motorcycle | | | Not roadworthy | ARUSHA |
| 21 | Not Seen | Motorcycle | Jianshe | 90cc | Not roadworthy | ARUSHA |
| 22 | MC250AAM | Motorcycle | | | Not roadworthy | ARUSHA |
| 23 | MC257AAM | Motorcycle | | | Not roadworthy | ARUSHA |
| 24 | MC171AGN | Motorcycle - | Yamaha Crux | | Scrap | MWANZA |
| 25 | MC180AGN | Motorcycle - | Yamaha Crux | | Scrap | MWANZA |
| 26 | MC382AHZ | Motorcycle | Yamaha YBR | | Scrap | MWANZA |
| 27 | MC181AGN | Motorcycle | Honda ACE | | Scrap | MWANZA |
| 28 | MC159AGN | Motorcycle- | Honda ACE | | Scrap | MWANZA |
| 29 | MC257AAM | Motorcycle | Toyo | | Not roadworthy | MWANZA |
| 30 | N/A | Motorcycle | Jianshe | 90cc | Not roadworthy | MWANZA |
| 31 | MC250AAM | Motorcycles | SANLG | | Not roadworthy | MWANZA |
| 32 | Not Seen | Motorcycle | Jianshe | 90cc | Not roadworthy | ARUSHA |
| 33 | MC250AAM | Motorcycle | | | Not roadworthy | ARUSHA |
| 34 | T542AHJ | Motor Vehicle | | | grounded | DSM |
| 35 | T637CLB | Motor Vehicle | | | grounded | DSM |
| 36 | T501AUF | Motor Vehicle | | | grounded | DSM |
| 37 | T576ART | Motor Vehicle | | | Offroad | DSM |
| 38 | T659 CKF | Motor Vehicle | | | Offroad | DSM |
| 39 | T902BUV | Motor Vehicle | | | Offroad | DSM |
| 40 | T606AXE | Toyota | Land Cruiser | | Not roadworthy | MWANZA |
| 41 | T606AXE | Toyota | Land Cruiser | | Not roadworthy | ARUSHA |
| 42 | T606AXE | Toyota | Land Cruiser | | Not roadworthy | MWANZA |
| 43 | | Generator | | | Used | MWANZA |
| 44 | Z538HH | Motorcycle | | | Used | ZANZIBAR |
| 45 | ZNZ44726 | Motorcycle | | | Used | ZANZIBAR |
| 46 | Z45323 | Motorcycle | | | Used | ZANZIBAR |
| 47 | Old Generator | | | | Used | ZANZIBAR |

**Condition of Sale:**

1. Vehicle are sold on **"AS IS WHERE IS"** basis GARDAWORLD shall note have further liability after sale
2. Viewing to verify details can be done during normal working hours (8.00am -4.00pm) at the location indicated.
3. Successfull bidder will be required to pay the full bid price within 2 working days from the date of the award
4. Successfull bidders will be required to remove purchased vehicle from site within 7 days from the date of award
5. Buyers will be required to un brand / repaint the vehicle within 7 days from the date the vehicles are handed over to them.
6. GARDAWORLD reserves all rights and without assigning any reasons there of not to accept the highest bid.
7. Bids can be placed in a sealed envelope marked **" TENDER FOR MOTOR VEHICLES"** and deposited at **GARDAWORLD OFFICES** Addressed to:

**FINANCE DIRECTOR**
**GARDAWORLD INTERNATIONAL**
**P.O.BOX 12747**
**DAR ES SALAAM**

**BRANCH MANAGER**
**GARDAWORLD INTERNATIONAL**
**P.O.BOX 2076**
**MWANZA**

**BRANCH MANAGER**
**GARDAWORLD INTERNATIONAL**
**P.O.BOX 12747**
**ARUSHA**


# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## Benki ya Exim Tanzania yaboresha mfumo wake mkuu wa kibenki ili kutoa huduma zilizo usalama, bora na ubunifu zaidi.

**[DAR ES SALAAM: MEI 11, 2023]**

BENKI ya Exim Tanzania imeboresha mfumo wake mkuu wa huduma za kibenki ikilenga kutoa huduma bora kwa wateja wake.

Kwa mujibu wa taarifa ya benki hiyo iliyotolewa mapema jana, mfumo huo mpya unarahisisha uchakataji wa miamala, hatua za usalama zilizoboreshwa, na utendaji kazi ulioimarishwa, ambao utahakikisha matumizi salama na rahisi zaidi ya benki kwa wateja.

Kupitia taarifa hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Bw. Jaffari Matundu, alisema kuwa mfumo huo mpya umeundwa ili kutoa suluhisho la huduma za kibenki kwa wateja hao na kuwawezesha kufanya miamala yao ya kifedha kwa urahisi na utulivu wa akili.

Aidha, Bw. Matundu alitoa shukrani zake kwa wateja wa benki hiyo kwa ushirikiano na uvumilivu wao wakati wa uboreshaji huo huku akiomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza kutokana na changamoto za mpito zinazojitokeza katika baadhi ya huduma kufuatia maboresho hayo.

Naye Ofisa Mkuu wa Teknolojia wa benki hiyo na Mkuu wa Kitengo cha Mabadiliko ya Kidijitali, Bw. Alamin Merchant, alisema mfumo huo ulioboreshwa, unatoa huduma na manufaa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na huduma za ziada za benki mtandaoni, taarifa (notifications) kwa wakati halisi, na programu ya huduma za benki kupitia simu ambayo ni rafiki na inayomfaa mtumiaji.

Bw. Merchant alionyesha shauku yake katika kuwapatia wateja suluhisho sahihi na huduma zilizoboreshwa hususani katika ufanyaji wa miamala, utendakazi ulioimarishwa, na hatua za usalama zilizoboreshwa.

Alisisitiza kuwa mfumo huo mpya umeundwa ili kufanya huduma za benki kufikiwa kwa urahisi zaidi na wateja sambamba na kuhakikisha kwamba akaunti zao na taarifa zao binafsi ziko salama kila wakati. Benki imejitolea kuendelea kuboresha huduma zake ili kukidhi mahitaji yanayoendelea ya wateja wake.

Katika kuhitimisha taarifa hiyo, Bw. Matundu alitoa shukrani zake kwa wateja kwa kuchagua Benki ya Exim kama mshirika wao wa kibenki na fahari yao katika teknolojia ya kisasa ya kibenki inayokidhi mahitaji yao yanayoendelea.

Aliahidi kuwa benki hiyo inaendelea kutoa uzoefu bora zaidi wa kibenki kwa wateja wake, na uboreshaji huo ni hatua muhimu ya kufikia lengo hilo.




Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot (kulia), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Alpha Mundi (AMF), Lade Araba (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Usaidizi wa biashara ndogo (SEAF) Peter Righi, wakikata utepe kuzindua mfuko wa kuwezesha wajasiriamali ujulikanao kama 'Daraja Impact Fund', nyumbani kwa balozi, Oysterbay jijini Dar es Salaam juzi, wenye lengo la kukuza biashara mbalimbali zilizopo kwenye mnyororo wa thamani kwa wajasiriamali wadogo, wanawake na vijana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aweso: Sasa tunayatoa maji ziwani hadi penye shida kuu

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso ametangaza kuwa serikali katika mwaka ujao wa fedha itajikita kutoa huduma penye shida kubwa, wakiyatoa maji ziwani na mito mikubwa, kuyapeleka penye uhaba mkubwa.

Pia ametaja mikakati yao mingine ni kuendelea na utunzaji wa nyanzo vya maji, kuimarisha usimamizi wa ubora wa maji, kukamilisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi inayoendelea kutekelezwa, ukiwamo wa miji 28.

Aliyasema hayo juzi bungeni jijini hapa alipopasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka 2023/24, akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 756.2 ili kutekeleza mikakati hiyo.

Waziri Aweso alisema wataendelea na ujenzi wa Bwawa la Kidunda na kuanza ujenzi wa Bwawa la Farkwa.

"Serikali imepanga kuendelea kuwekeza katika utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kuweka mipaka inayoainisha maeneo ya hifadhi katika vyanzo vya maji, ili kudhibiti shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo na mengine kuyatangaza katika Gazeti la Serikali kama maeneo tengefu," alisema Aweso.

Waziri huyo alisema kuwa katika mwaka 2023/24, vyanzo vya maji 84 vitawekwa mipaka na kutangazwa kama maeneo tengefu.

Kuhusu ujenzi wa mabwawa, Aweso alisema wataendelea kuimarisha mfumo wa uvunaji maji ya mvua na kuanza utekelezaji wa ujenzi wa bwawa moja kwa kila wilaya yenye mazingira yanayofaa. Alisema wataongeza kasi ya ujenzi wa mabwawa ya maji ya ukubwa wa kati hususani katika maeneo yenye ukame kwa kujenga mabwawa ya kimkakati.

"Tutajenga mabwawa 27 ya ukubwa wa kati na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa mabwawa ya ukubwa wa kati kwa ajili ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua," alisema Aweso.

Waziri Aweso alisema pia watakarabati vituo 135 na kujenga vipya 51 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji, kutoa vibali 450 vya matumizi ya maji, vibali 30 vya kutupa majitaka, kuunda jumuiya 10 za watumia maji pamoja na kuzijengea uwezo jumuiya 87 na kuunda kamati tisa za vidakio. Vilevile, alisema wataendelea kusimamia shughuli za uchimbaji wa visima vya maji, kuendesha majukwaa na vikundi kazi vya wadau wa sekta mtambuka wa rasilimali za maji.

Alisema kuwa kwa mwaka 2023/24, wataendelea kuimarisha uhakiki na ufuatiliaji wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji 2,091, skimu 4,600 za usambazaji maji mijini na vijijini pamoja na mifumo 150 ya majitaka.

Waziri Aweso alisema katika mwaka 2023/24 watatekeleza miradi ya maji 1,546 maeneo ya vijijini, 244 mijini pamoja na ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhi maji katika maeneo mbalimbali.

Alisema: "Tutatekeleza miradi mikubwa itakayotumia vyanzo vya uhakika. Katika mwaka 2023/24, serikali itafanya mapitio ya usanifu wa mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara - Mikindani pamoja na vijiji na vitongoji vilivyopo ndani ya kilomita 12 ya bomba kuu".

Aliongeza: "Pia tutafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi wa kutoa maji Mto Rufiji kupeleka Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Mkoa wa Pwani na kuanza ujenzi wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi miji ya Malampaka na Malya."

# Ajali ya bodaboda mbili ilivyoua diwani

**Na Gideoni Mwakanosya,** SONGEA

WATU wawili, akiwamo Diwani wa Mtyangimbole katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba mkoani Ruvuma, Erick Herman Mkolo (48), wamefariki dunia na wengine wawili kujeruhiwa baada ya pikipiki walizokuwa wakiziendesha kugongana uso kwa uso.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake mjini hapa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Marco Chillya, alisema tukio hilo lilitokea juzi saa 1.30 usiku katika Kijiji cha Mlilayoyo Mageuzi, Wilaya ya Namtumbo, barabara kuu Songea-Njombe.

Kamanda Chillya alisema pikipiki zenye namba za usajili MC 988 CMN, na MC 812 DLF, zote aina Haojue, zilizokuwa zinaendeshwa na Diwani Mkolo na Siraju Sawmba (23), mkazi wa Bombambili, Manispaa ya Songea, ziligongana uso kwa uso na kusababisha waendesha pikipiki wote kufariki dunia huku abiria wao wakijeruhiwa.

Aliwataka abiria hao ni John Mkinga (39), mkazi wa Kijiji cha Lutikila, Jimbo la Madaba na Aurito Carlos (33) ambaye inadaiwa ni raia wa Msumbiji.

Kamanda huyo alisema kuwa kutokana na ajali hiyo, kumetokea uharibifu mkubwa wa vyombo vyote viwili. Chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi kwa waendesha pikipiki wote wawili na kutoheshimu sheria za usalama barabarani.

Alifafanua kuwa Diwani Mkolo alikuwa akitokea Kijiji cha Likarangilo kwenda mjini Songea na aligongana na Sawamba aliyekuwa anatoka mjini Songea kwenda Mtyangimbole.

Kamanda Chillya alieleza kuwa majeruhi wote wawili wamelazwa katika Hospital ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma ambako wanaendelea na matibabu.

Aliwataka waendeshaji wa vyombo vya moto na watumiaji wengine wa barabara kuzingatia sheria zilizowekwa ili kuepusha ajali zinazosababisha vifo, majeraha na uharibifu wa miundombinu.

# ...Hasunga: Tuwe na gridi ya maji

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WABUNGE wamelalamika kuchelewa kukamilika kwa wakati miradi ya maji, wakiishauri serikali kuanzisha gridi ya maji kama ilivyo katika umeme ili kumaliza tatizo la ukosefu wa huduma hiyo katika maeneo mengi nchini.

Katika mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka ujao wa fedha bungeni juzi na jana, wabunge hao walisema miradi mingi ya maji inatekelezwa kwa zaidi ya miaka miwili, mingine ikitelekezwa na makandarasi pasipo kutolewa taarifa yoyote.

Mbunge wa Vwawa (CCM), Japhet Hasunga, alisema maji ndiyo maisha, uhai, chakula, nishati na usalama wa wananchi na Tanzania imebahatika kuwa na mabonde, mito na maziwa, hivyo wananchi wake hawastahili kulia kili siku kwa ukosefu wa maji au shida ya maji.

"Kilichobaki tuje na mpango mzuri wa matumizi ya maji wa muda mrefu. Kwa sasa tuna miradi mingi kila mahali inatekelezwa. Lazima tuwe na mpango utakaodhibiti matumizi bora ya maji na tuwe na gridi ya maji kama ilivyo katika umeme," alisema Hasunga.

Alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji wa miradi mingi ya maji ikiwamo ya jimboni kwake. Hata hivyo, aliitaka wizara kusaidia upatikanaji wa maji katika jimbo hilo kwa kuwa kwa sasa uko chini ya asilimia 50.

"Ukiangalia wilaya inavyozalisha katika nchi hii, ukiangalia namba wananchi wanavyofanya kazi. Kwa kweli, uhaba wa maji kule haukubaliki kabisa. "Mheshimiwa Waziri, ninakuomba kama kaka yako, hebu lifikirie Jimbo la Vwawa. Hebu iangalie Wilaya ya Mbozi utatue changamoto ya uhaba wa maji," alisema na kusisitiza hatopenda kuwa mbunge wa kulialia bungeni.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Agnes Hokororo, alisema: "Wizara haina namna ni muhimu ikatengeneza mpango wa maji na kuwa na gridi ya maji. Unganisha vyanzo vikubwa vya maji kwa maana ya maziwa na mito mikubwa ndipo utaona lengo la Rais Samia kumtua mama ndoo kichwani linafanikiwa."

Mbunge wa Bunda (CCM), Boniphace Getere, akizungumzia upotevu wa maji, alisema viwanda vinavyotengeneza mabomba hayako katika viwango vinavyotakiwa kwa kuwa baada ya kutumiwa kwa muda mfupi yanapasuka.

Mbunge wa Mpwapwa (CCM), George Malima, alisema kuna baadhi ya miradi ya maji katika jimbo lake haijatekelezwa kwa zaidi ya miaka miwili sasa.

Aliutaja mradi wa kuchimba visima virefu jimboni kwake ambao kila mwaka unatengewa fedha lakini hautekelezwi, hivyo akaitaka serikali kuutekeleza.

Mbunge wa Moshi Vijijini (CCM), Prof. Patrick Ndakidemi, alisema maeneo mengi ya Moshi Vijijini hayana huduma ya maji.

Alisema eneo Uru Kusini, kuna wakazi zaidi ya 31,000 lakini wanaoishi Kata ya Kisiweni, Mang'anga hawana huduma ya maji kwa muda mrefu. Ndakidemi alisema eneo la Arusha Chini lina wakazi zaidi ya 19,000 lakini vijiji vya Mikocheni na Chemichemi vinakabiliwa na ukosefu wa huduma ya maji.

Mbunge wa Ulyankulu (CCM), Rehema Migila alisema mradi wa Bwawa la Ichemba ulitengewa Sh. milioni 750 lakini hadi sasa hakuna kazi yoyote inayoendelea. Pia alisema Mradi wa Katapila ulitengewa Sh. bilioni 25 lakini ni zaidi ya miaka miwili sasa hakuna utekelezaji wowote na mkandarasi hayuko eneo la mradi. Mbunge wa Kilombero (CCM), Abubakar Asenga, alisema jimboni kwake kuna mradi wa Kiburungutu ambao umechukua zaidi ya mwaka kukamilika.

Mbunge wa Chemba (CCM), Mohamed Monni, alilalamika miradi mingi ya Chemba haijakamilika na kumtaka Waziri wa Maji, Jumaa Aweso awafuatilie makandarasi na kuwaondoa.

"Ni lazima kuwe na uwiano wa upatikanaji maji. Haiwezekani jimbo fulani wanapata maji asilimia 36 wengine asilimia 80. Lazima kuwe na mpangilio wa kugawana rasilimali za nchi yetu," alisema Monni.

Mbunge wa Viti Maalum, Stella Fiyao, alisema eneo la Momba vijiji takribani 50 havina maji.

"Hiyo asilimia 70 ya upatikanaji wa maji vijijinI Waziri Aweso unaitoa wapi? Katika karne hii wananchi kweli wanachangia maji na mifugo? Ndiyo sababu homa ya matumbo haishi. Ninataka waziri aje atueleze mikakati yake kuhakikisha wananchi wanapata maji salama," alisema.

# MATANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TANGAZO KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YALIYOWASILISHWA NA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA ROMBO (ROMBO WSSA)

Mnamo tarehe 3 Aprili 2023, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea maombi ya marekebisho ya bei za maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo (Rombo WSSA). Majedwali Na 1 hadi 3 yanaonesha viwango vya bei vinavyopendekezwa na Rombo WSSA.

**Jedwali 1: Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)**

| Kundi la Wateja | | Bei ya Sasa | Bei zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 0-5m$^3$ | 800 | 1,362 | 1,429 | 1,465 |
| | >5m$^3$ | 900 | 1,455 | 1,527 | 1,566 |
| Taasisi | | 900 | 1,532 | 1,607 | 1,648 |
| Biashara | | 1,200 | 1,838 | 1,929 | 1,978 |
| Maosheo ya Magari | | 2,000 | 2,724 | 2,858 | 2,931 |
| Magati | | 1,000 | 1,447 | 1,518 | 1,557 |
| Shule za Umma | | 800 | 1,062 | 1,114 | 1,143 |
| **Weighted Average Tariff** | | **900** | **1,532** | **1,607** | **1,648** |

**Jedwali 2: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shlingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Wateja Wote | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |

**Jedwali 3: Ada ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kuunganishiwa Huduma (Shilingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | Asilimia 20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | Asilimia 20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |

Rombo WSSA imeeleza kuwa bei na ada zinazopendekezwa zitaiwezesha kutekeleza shughuli zilizoainishwa kwenye mpango biashara wake kwa kipindi cha kuanzia 2023/24 hadi 2025/2026 ili kuleta uendelevu wa utoaji huduma za maji. Hasa, kuisaidia mamlaka kurejesha gharama za uendeshaji na matengenezo pamoja na kukidhi gharama za ukarabati, ubadilishaji na uwekezaji mpya na hivyo kutoa maji ya kutosha, safi na salama katika eneo la huduma ya mamlaka, kubadili miundombinu chakavu ya maji, kupanua mtandao wa maji, kununua vitendea kazi na mali nyingine muhimu, kuongeza idadi ya wateja na idadi ya watu inayohudumiwa moja kwa moja na maji.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 18 Mei 2023, katika Ukumbi wa Gosheni uliopo Mkuu, Rombo kuanzia saa 4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la Watumia Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC) na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaombwa kuwasilisha maoni ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kupitia anuani iliyotajwa hapo juu wakati wowote hadi tarehe 25 Mei 2023. Maelezo zaidi kuhusu maombi ya Rombo WSSA yanaweza kupatikana kwenye ofisi za **Makao Makuu ya EWURA** zinazopatika katika **Jengo la EWURA, 3 Barabara ya EWURA, 41104 Tambukareli, Dodoma au Ofisi za EWURA Kanda ya Kaskazini zilizopo Ghorofa ya Pili, Jengo la PSSSF, Jirani na Kibo Palace Hotel, Arusha Mjini.**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

## TANZANIA COMMISSION FOR UNIVERSITIES

## REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST

**Country:** TANZANIA
**Name of Project:** Higher Education for Economic Transformation (HEET)
**Credit No:** IDA- 68870
**Project ID No:** P-166415
**Assignment Title:** Provision of Consultancy Services for Undertaking Environmental and Social Impact Assessment (ESIA) for Construction of the proposed TCU Headquarters Building on Plot No. 56/4, Block E, Kisasa B Area, Dodoma City.

**Reference No.: PA/073/WB-HEET-P-166415/350608/2022-23/CS/01**

1. The Government of the United Republic of Tanzania through the Ministry of Education, Science and Technology (MoEST) has received financing from the World Bank to meet the costs for implementation of the Higher Education for Economic Transformation (HEET) Project and intends to apply part of the proceeds of this fund to cover eligible payments under the contract for Provision of Consultancy Services.

2. The consulting services ("the Services") include carrying out the Consultancy Services for undertaking Environmental and Social Impact Assessment (ESIA) for the Proposed Construction of Tanzania Commission for Universities office building in Dodoma. The total duration for the entire assignment shall be three (3) months. The estimated level of effort is ninety (90) person days.

3. The detailed Terms of Reference (ToR) for the assignment are available in the following website "**www.tcu.go.tz**" or can be obtained at the address given below.

4. The Tanzania Commission for Universities now invites eligible consulting firms ("Consultants") to indicate their interest in providing the Services. Interested Consultants should provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the services. The shortlisting criteria are:

   **A. Core business of the firm and five (05) years in business**

   **B. Relevant similar experience, which should specifically include the following;**
   i. Experience of at least three (3) Environmental and Social Impact Assessment as assignments in the last ten (10) years and above – Information to be provided should include name of assignments, names and full contact addresses of the Clients, contract value (in equivalent US dollars) and period (dates) of execution of assignments.
   ii. Demonstration of experience of work in similar conditions.

   **C. Technical and managerial capability of the firm**
   The Consultant must provide the structure of the organization, general qualifications and number of Key staffs. (Do not provide CV of the Key staff. Key Experts will not be evaluated at the shortlisting stage).

5. Attention of interested Consultants is drawn to Section III, paragraphs, 3.14, 3.16, and 3.17 of the World Bank's "Procurement Regulations for IPF Borrowers" Fourth Edition of November, 2020 ("Procurement Regulations"), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.

6. Consultants may associate with other firms to enhance their qualifications, but should indicate clearly whether the association is in the form of a joint venture and/or a sub-consultancy. In the case of a Joint Venture (JV), all the partners in the joint venture shall be jointly and severally liable for the entire contract, if selected. Therefore, each member of JV shall independently meet the requirements of the evaluation criteria. The experience, technical and managerial capability of the Sub-Consultant shall not be evaluated to enhance the qualifications of the Lead Firm or JV.

7. A Consultant will be selected in accordance with the **Consultant's Qualification Selection (CQS)** method set out in the Procurement Regulations.

8. Further information can be obtained at the address below during office hours 08:00 – 15:30 Hours East African Time on Monday to Friday inclusive except on public holidays.

9. Expressions of interest should be submitted online through Tanzania National Electronic Procurement Systems (TANePS) (www.taneps.go.tz) on or before 30th May, 2023 at 10:00 Hour's East Africa Time. The Client shall not be held liable for any delays due to system failure beyond its control. Even though the system will attempt to notify the Consultants of any updates, the Client shall not be liable for any information not received by the Consultants. It is the Consultants' responsibility to verify the website for the latest information related to this selection process. Expression of Interests will be opened promptly through TANePS.

**EXECUTIVE SECRETARY**
**TANZANIA COMMISSION FOR UNIVERSITIES**
**P.O. BOX 6562**
**DAR ES SALAAM**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wabunge wasimamie, waheshimu miongozo na kanuni walizojiwekea/ wanachokitunga

**BUNGE** linaendelea na mkutano wake mjini Dodoma kwa ajili ya kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara mbalimbali kabla ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2023/24.

Mpaka sasa tayari wizara kadhaa zikiwamo ofisi za Rais na Waziri Mkuu zimeshawasilisha makadirio yao. Baada ya kukamilika kwa makadirio ya wizara hiyo, ndipo Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, atawasilisha bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha ambayo itaweka bayana vipaumbele kwa mwaka husika na maeneo ya vyanzo vya mapato ambavyo vitasaidia katika utekelezaji wa bajeti hiyo ikiwamo miradi ya maendeleo.

Sambamba na wabunge kujadili na kupitisha makadirio ya wizara hizo, pia wanapata nafasi ya kuuliza maswali ili kupata majibu ya kero zilizoko kwenye majimbo yao na sehemu zingine. Aidha, kila Alhamisi, wabunge wanapata fursa ya kumuuliza maswali Waziri Mkuu ambayo mengi ni ya kisera zaidi.

Wakati yote hayo yakiendelea, wiki hii, Mbunge wa Tarime Vijijini (CCM), Mwita Waitara, alifanya kituko cha mwaka wakati wa kipindi cha maswali na majibu kwa kile alichodai ni kutokuridhishwa na majibu ya swali alilouliza. Mbunge huyo ambaye ni kipindi chake cha pili na alishakuwa Naibu Waziri katika serikali ya awamu ya tano, alivua tai na koti kisha akatoka nje.

Hatua hiyo ilimfanya Spika wa Bunge, Tulia Ackson, kupokea mwongozo na kulitolea majibu suala hilo huku akisisitiza kwamba kanuni za kudumu za bunge haziruhusu mbunge kuvua nguo akiwa bungeni na kuweka bayana kwamba kitendo alichofanya Waitara ni cha utovu wa nidhamu. Bila kuuma maneno, Dk. Tulia aliweka bayana kuwa kanuni za bunge hazitoi nafasi asilani kwa mbunge kufanya kituko cha aina yoyote kama alivyofanya Waitara.

Kitendo alichokifanya mbunge huyo kimeonyesha ni namna gani wabunge wanavyokiuka kanuni na miongozo iliyowekwa katika kusimamia wawapo katika chombo hicho kwa ajili ya kuwawakilisha wapigakura wao kujadili na kuzitafutia ufumbuzi kero zinazowahusu wananchi katika maeneo yao ya uwakilishi.

Kwa kawaida, mbunge anapouliza swali la msingi na kujibiwa na serikali, ana nafasi ya kuuliza angalau maswali mawili ya nyongeza ili kupata undani wa kile anachotaka. Waitara badala ya kufanya hivyo, aliamua kuvua koti na tai na hatimaye kwenda nje ya ukumbi wa bunge. Kwa ujumla, kitendo hicho kimeonyesha baadhi ya wabunge wanavyoshindwa kusimamia kanuni zinazowaongoza ambazo wamezitunga wenyewe.


Miaka kadhaa iliyopita, wananchi waliliona bunge ni kama sehemu ya watu kupiga porojo na kufanya mipasho kutokana na vijembe vilivyokuwa vimetawala wakati wa shughuli mbalimbali za chombo hicho. Kwa kilichotokea wiki hii, kimesadifisha dhana hiyo na kuwafanya baadhi ya wananchi kuamini kwamba wabunge wanaingia katika mhimili huo wa kutunga sheria kwa maslahi binafsi.

Bunge ni chombo kinachoheshimika kutokana na nafasi yake katika mwelekeo na hatima ya nchi kwa sababu ndiyo taasisi ambayo imepewa jukumu la kutunga sheria, kupitisha bajeti na kuishauri serikali juu ya masuala yanayopitishwa. Sasa kama bunge lenyewe haliwezi kusimamia kile ilichokitunga. Watu wengine watakuwaje radhi kutekeleza maelekezo na maazimio yake?

Kuwapo kwa vitendo kama hivyo kunadhihirisha wazi kutokuwapo kwa umakini kwa baadhi ya wabunge na matokeo yake kushindwa kutunga sheria nzuri kwa maslahi ya taifa.

Pia kitendo kama cha Waitara, kinaibua maswali mengi ikiwamo kama ni kweli huwa wanakaa, kusoma na kupitia kwa kina masuala yanayowasilishwa ikiwamo miswada ya sheria ili kutoka na sheria bora badala ya bora sheria?.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Christina Mwakangale

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera LATRA ubunifu safari za mijini, ila mnapofeli hapa

**UKWELI** bayana, daladala kwa miji yote inafanya kote kufikike saa zote, hata usiku wa manane. Tafakari, eneo la Buguruni mkoani Dar es Salaam, ni kati ya vituo maarufu mwanzo wa safari ndani mjini hapo, kwenda kokote saa 24.

Pongezi kwa iliyokuwa ikisimamia usafiri, ikijulikana SUMATRA, yaani Mamlaka ya Usafiri wa Majini na Nchi Kavu, kisha ikazaliwa LATRA, Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu, iliyobuni ruti za mijini kila kona.

Huwezi kuweka kando mafanikio hayo, bila kumtaja David Mwaibula, mbunifu wa miaka ya 2000, kupakwa rangi tofauti daladala kwa kila ruti, hatua iliyosaidia hata wasiojua kusoma, wakiona daladala utambulisho wa rangi unafanya kazi yake.

Mwaibula ni miongoni mwa wachache waliofanikisha wazo kwa kutatua changamoto za kijamii kama ilivyo usafiri wa treni daladala maarufu 'treni ya Mwakyembe' kwenye TRC na TAZARA, mkoani Dar es Salaam, wakatumia huduma zao kuokoa uhaba wa usafiri wa umma.

Najua, zipo changamoto kwa mamlaka na wasimamizi wa usafiri wa umma mijini wanazipata kuhakikisha mawazo yaliyobuniwa na yanayobuniwa, yanaishi kwa kuboreshwa.

Mfano madereva wa daladala na makondakta wao, wanahitajika kuvaa sare kwa mujibu wa kanuni za usafiri wa umma. Hiyo ni muhimu, ikiondoa mkanganyiko wa aliye abiria au mfanyakazi wa gari, akiwamo kondakta 'mtoza fedha'.

Utakutana na watoa huduma hao, hasa makondakta, wanaovaa mkono mmoja wa shati au suruali, imechanika, suruali haina zipu wala vifungo, muda wowote inaweza kumvuka.

Na joto linavyozidi kwenye miji mingi kutokana na mabadiliko ya tabianchi, wavaaji sare hizo, kiukweli hawazifui na zinatoa harufu, pia uvundo. Inavyoonekana hivi sasa hata usimamizi katika hili umepungua, pengine kutokana na LATRA kupunguza kasi.

Msafiri kafiri! Walijisemea wahenga. Ni usafiri unaoonekana kama 'bora liende'. Utakuta daladala chafu, kifaa cha kuwekea taka au 'dustbin' ndani ndio balaa, usiombe ukutane kinaning'inia juu ya kiti ulichokaa au ulikosimama, au jirani na kichwa chako.

Sare za makondakta inaelekea ziko pea moja tu, madai ni zinauzwa ghali huko VETA zinakopatikana. Mbaya zaidi ni 'free size' yeyote anavaa hata 'madei waka'.

Zinavaliwa chafu, Jumatatu hadi Jumatatu nyingine, sasa 24, siku 365 za mwaka hakuna mabadiliko. Ukiwatazama, wengi hawapendi kuzivaa, utaona kiuno cha suruali ndio shida, anaweza akavaa yeyote; mnene au mwembamba!

Shati nalo lina kasoro hizo hizo, hakuna vifungo, ni nadra au huwezi kumwona kondakta au dereva kavaa kistaarabu, au kupendeza, zikiwa ni kero kwa abiria, hasa kondakta anapobanana na abiria akidai nauli. Kila mmoja anajitahidi kutoa nauli haraka, akiangalia pembeni au kujifanya hajamsikia kondakta, ili kuepukana na harufu ya nguo hizo.

Niseme, jamii haipaswi kulikalia kimya, ni huduma kama nyingine za umma. Uvaaji sare upo kulingana na sheria, kanuni na taratibu za usafirishaji katika usafiri wa umma.

Wanafunzi wa shule, polisi, wanajeshi, Idara ya Uhamiaji, watumishi wa baadhi ya taasisi, mamlaka, wahudumu wa vituo vya mafuta, walinzi wa kampuni binafsi na kwingineko huvaa tena zikiwa safi na rangi zinazoshabihiana, hadi viatu viko nadhifu.

Heshima ya kazi huanzia na mtu mwenyewe, ndipo mwingine ataiheshimu, mtindo wa kuvaa nguo isiyo nadhifu, shati kubwa, suruali inayoning'inia miguuni, ikiwa na makunyanzi, achilia mbali uchafu wake, kuonana na maji ni kama mtu na mkwewe zama zile.

Dunia inavyokua inahitaji mabadiliko kila sekta na binadamu kuongeza ustaarabu kwa namna anavyoishi. Daladala zinakuwa hata na wadudu wasiofaa na hatari kwa afya za abiria; mbu, mende, kunguni ikikosa vitunzia taka 'dustbin'.

Mathalani, wiki hii nikiwa ndani ya daladala kutoka Makumbusho hadi Pugu Stesheni, nilikuta maajabu kuanzia mlangoni, viti vyake hadi kondakta ni uchafu mtupu. Nikajiuliza, gari hili linatumiwa na abiria au kusafirisha taka au mifugo, kutokana na uhalisia wake?

Nitoe rai, wenye dhamana, ukaguzi wa magari haya usiishie nje tu, iwe hadi ndani , utakutana na vyuma vilivyojitokeza au mabati chakavu hatari kwa abiria.

HABARI KITAIFA

# Tanzania kuwa kitovu cha tiba Afrika

**Na Joseph Mwendapole**

UWEKEZAJI mkubwa ambao umefanywa na serikali kwenye miundombinu ya hospitali na vifaa tiba vya kisasa, unakusudia kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii wa tiba kwenye ukanda wa kusini mwa Jangwa la Sahara.

Tanzania imekuwa moja ya nchi zinazoongoza kusini mwa jangwa la Sahara kwa kutoa huduma bora za tiba kulinganisha na mataifa mengine, hivyo kuanza kupokea wagonjwa kwenye mataifa mbalimbali.

Hayo yalisemwa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Dk. Mohamed Janabi, wakati wa uzinduzi wa Kamati za Utalii Tiba za MNH, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Mifupa (MOI) na Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI).

Dk. Janabi ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii Tiba Kitaifa, alisema uwekezaji huo umeifanya Tanzania kuwa na nafasi nzuri ya kunufaika na utalii wa tiba kwa wagonjwa wa mataifa mbalimbali kuja kutibiwa hapa nchini.

Mkurugenzi wa Magonjwa ya Nje Wizara ya Afya, Dk. Asha Mahita, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi huo, alipongeza kazi kubwa iliyofanywa na wajumbe wa Kamati ya kitaifa ya utalii wa tiba tangu wateuliwe.

Alisema imechukua muda mrefu dhana ya utalii wa tiba kufahamika hasa kwenye hospitali za hapa nchini akisema kuwa utalii wa tiba utasaidia kwa kiwango kikubwa kuongeza mapato ya serikali kwa wageni watakaokuja.

Pamoja na kuongeza mapato kutokana na utalii wa tiba, alisema hata watu binafsi watakuwa wakinufaika kwa kuleta wagonjwa kutoka mataifa mbalimbali na hospitali husika itakayopokea wagonjwa hao itanufaika.

"Dhana ya utalii wa tiba ni pana mno na inahitaji uzalendo sana kama mwenzetu Abdulmalik Mollel na kampuni yake ya Global Education Link, uzalendo ni kuisaidia serikali katika majukumu mbalimbali na moja wapo ni kama hili," alisema.

"Kwa hiyo tunatarajia watajitokeza wadau mbalimbali kama Mollel kuhakikisha hili gurudumu la utalii wa tiba linakwenda mbali zaidi . Serikali haiwezi kufanya kazi hii peke yake ndiyo sababu wakati Waziri anaiunda hii kamati alishirikisha sekta binafsi kwasababu hata vifaa vya hospitali binafsi vinahitajika kwenye huu utalii wa tiba," alisema.

Dk. Mahita alisema Wizara ya Afya inaandaa mwongozo ambao utaeleza majukumu ya kamati na kila mtu ili kuhakikisha kila mtu anatimiza wajibu wake na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

"Rai yangu kwa Kamati ya Utalii ni kwamba kazi bado mbichi sana. Kushindwa kwenu ni aibu ya serikali kwa hiyo hatuwezi kuona mnashindwa hii kazi wakati wajumbe wote wa kamati ni watu wenye weledi wa hali ya juu, tutatafuta fedha ila tukikosa itabidi mjitolee tu," alisema. Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk Peter Kisenge, alipongeza kamati hiyo na kusema maono ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii wa tiba yanaonekana kuanza kutimia kutokana na kazi kubwa ambayo imefanwa na Kamati hiyo.

"Sisi JKCI tumeanza safari ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii wa tiba Afrika na tumeshapeleka madaktari wetu kwenye nchi mbalimbali kama Comoro na Malawi na tunatarajia kwenda Burundi na Congo siku chache zijazo. Tumeweka mipango ya kutekeleza maono ya Kamati ya Utalii," alisema.



Mkurugenzi wa Magonjwa ya Nje Wizara ya Afya, Dk. Asha Mahita (katikati), akikabidhi ripoti kuhusu utalii tiba kwa Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, katika uzinduzi wa Kamati ya Utalii Tiba, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni wajumbe wa kamati hiyo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE.**

# Bandari kuongeza uwezo kupokea shehena

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), inatarajia kujenga magati matatu likiwamo la kupokea makontena (makasha) na kuifanya kuwa na uwezo wa kuyapokea kufikia milioni 2.5.

Pia inatarajia kujenga gati maalum ya kuhudumia watalii na ya kuegesha meli za abiria.

Hayo yalisemwa jana Dar es Salaam katika mkutano wa siku tatu, uliolenga kupitia mradi huo ulioko kwenye hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu.

Mkutano huo ambao ulifungwa jana ulikutanisha wadau mbalimbali wa bandari, TPA yenyewe na wataalam washauri waelekezi kutoka kampuni ya Khatib & Alami (KA), ambayo ndiyo mshauri wa mradi huo.

Wataalam hao waliwapitisha hatua kwa hatua ya utekelezaji wa mradi huo na wadau wa sekta mbalimbali walikutoa ushauri wao na kupokelewa kwa ajili ya hatua nyingine.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Kaimu Mkurugenzi wa Mipango ya Miundombinu na Uwekezaji wa TPA, Ntandu Mathayo, ambaye ni Meneja Mradi huo, alisema kwa sasa mamlaka inafanya maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam kwa kuiboresha miundombinu iliyopo na kuongeza mingine.

"Maboresho yanayofanyika sasa yanatakayofanywa yanaifanya bandari kuwa na uwezo wa kuhudumia mzigo hadi kufikia tani milioni 28. Baada ya miaka 10 ijayo uwezo huo utafikiwa. Ili kujiandaa na mzigo unaokuja siku zijazo ndio maana tunataka kujenga gati la kupokea meli za makasha.

"Kwa sasa maboresho yanayofanyika bandari itakuwa na uwezo wa kubeba makasha 1, 150,000 baada ya miaka 10 ijayo tunatarajia mzigo utaongezeka. Ukiangalia miaka 12 iliyopita 2012 mpaka 2022 shehena la makasha limeongezeka kwa asilimia 110," alisema.

Alisema mwaka 2012 mzigo uliobebwa wa makasha kupitia bandari ya Dar es Salaam ulikuwa makasha yasiyozidi 450,000 na mwaka 2022 yalikuwa zaidi ya 880,000.

Mathayo alisema gati linalotarajia kujengwa hivi karibuni kutokana na upembuzi yakinifu unaofanywa na wataalam hao, litaongeza uwezo wa bandari wa kubeba makasha 1,350,000.

"Kwa maana hiyo ukichukua uwezo wa sasa wa bandari na baada ya kujengwa kwa gati hili, tutakuwa na uwezo wa kuhudumia kontena milioni 2.5.

"Teknolojia itakayotumika kwa sasa vifaa tunavyotumia kuhudumia mizigo bandarini vinatumia mafuta ya dizeli. Kwa kuzingatia hali ya mazingira duniani ambayo ndio ajenda kubwa ya mabadiliko ya tabia nchi, tunatarajia vifaa vyote vinavyohudumia makasha vitatumia teknolojia mpya ya umeme," alisema.

Kuhusu gati ya kuhudumia meli za watalii alisema kwa sasa bandari haina miundombinu hiyo na kutokana na nia ya serikali kuufanya mji wa Dar es Salaam kuwa wa kitalii, TPA imeamua kuijenga ili kuhudumia maeneo yote yanayozunguka jiji hilo zikiwamo mbuga za wanyama na visiwa vya Zanzibar na Pemba. Alisema ujenzi wa gati utategemea na ushauri watakaopokea kutoka kwa mtaalam huyo mwelekezi anayefanya upembuzi yakinifu.

Meneja Mradi kutoka KA, Chadi Sabra, alisema wao ndio wanaosimamia ujenzi wa magati 12 mpaka 15 ya kusimamia meli.

"Tumefanya mkutano huu ambao umeisha leo ukihusisha mazungumzo na TPA kwamba ni vitu gani vinahitajika na tumewapa ripoti. Ila tumekutana na wadau hawa kote nchini kuwaambia vitu gani vinahitajika," alisema.

Hata hivyo, alisema wanafanya kazi kwa karibu na TPA kuhakikisha bandari ya Dar es Salaam inaongeza mzigo na kuliweka jiji hilo kuwa kituo cha utoaji huduma hiyo kwa ubora ndani na kwa nchi inazoizunguka.

Meneja wa kampuni hiyo upande wa Tanzania, Gloria Mushi, aliishukuru TPA kwa kuwaamini na kwamba wamekutana na wadau tofauti wakiwamo Wizara ya Utalii, Shirika la Reli Tanzania (TRC), Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na Wizara ya Fedha na Mipango.

Mwakilishi wa Katibu Mtendaji wa Shoroba ya Kati, Faraja Kondo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kufanya maboresho ya bandari na kuwataka wadau waendelee kuitumia Bandari ya Dar es Salaam.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



BancABC part of atlasmara

# TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### TAARIFA YA UKAGUZI WA WARAKA MIZANIA KWA MWAKA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31 Dec 21 | Mwaka uliopita 31 Dec 20 |
|---|---|---|
| **A MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 4,679 | 2,911 |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 11,488 | 12,287 |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 43,956 | 43,436 |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 107,088 | 114,554 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 125,843 | 129,669 |
| | - | - |
| 12 Mali Nyingine | 18,094 | 25,189 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 5,217 | 6,342 |
| **16 JUMLA YA MALI** | **317,365** | **335,386** |
| **B DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 69,841 | 69,416 |
| 18 Amana za Wateja | 138,954 | 132,293 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 Amana Maalumu | - | - |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 Dhima Nyingine | 4,229 | 6,352 |
| 28 Madeni | 92,809 | 100,354 |
| **29 JUMLA YA DHIMA** | **305,833** | **308,414** |
| **30 MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **11,531** | **26,972** |
| **C FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 105,114 | 105,114 |
| 32 Hisa za Upendeleo | 17,840 | 17,840 |
| 33 Akiba ya Mtaji | - | - |
| 34 Hifadhi ya hatari ya benki kuu | - | 2,163 |
| 35 Mapato Yaliyobakizwa | (114,441) | (99,134) |
| 36 Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,018 | 989 |
| **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **11,531** | **26,972** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 1,945 | 674 |
| 39 Mikopo Chechefu | 7,265 | 16,315 |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 6,412 | 11,862 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 3.63% | 8.04% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.49% | 11.53% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 63.34% | 70.17% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 41.67% | 42.20% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 49.24% | 49.00% |
| (vi) Ongezeko la Amana | 5.04% | 15.91% |
| (vii Ongezeko la Mali | -5.37% | 0.18% |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31 Dec 21 | Mwaka uliopita 31 Dec 20 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 40,899 | 40,620 |
| 2 Gharama za Riba | (19,878) | (20,403) |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **21,020** | **20,217** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (4,943) | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (1,150) | - |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **9,021** | **4,926** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 905 | 931 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 8,116 | 3,995 |
| 6.3 Gawio | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(30,681)** | **(34,221)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (10,991) | (10,309) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (1,642) | (1,569) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (18,048) | (22,343) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(6,733)** | **(9,078)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (10,537) | (279) |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(17,270)** | **(9,357)** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | 2,029 | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(15,241)** | **(9,357)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 177 | 167 |
| 14 Mapato kwa Hisa | -164% | -89% |
| 15 | 0% | 0% |
| 16 Idadi ya Matawi | 6 | 6 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -2.12% | -2.71% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -58.39% | -33.66% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | -102.13% | -136.11% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.86% | 1.75% |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA DESEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31 Dec 21 | Mwaka uliopita 31 Dec 20 |
|---|---|---|
| **I Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (6,733) | (9,078) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| - Hasara Katika Mali | 3,759 | 3,718 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,267) | 4,285 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 7,087 | (19,295) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (520) | (258) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (2,123) | 3,537 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 7,427 | 6,049 |
| - Kodi Iliyolipwa | (243) | (279) |
| - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **6,386** | **(11,321)** |
| **II Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (5,337) | (6,881) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(5,337)** | **(6,881)** |
| **III Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (7,544.79) | 25,713.24 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(7,545)** | **25,713** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (6,496) | 7,511 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 129,751 | 122,240 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **123,255** | **129,751** |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(99,334)** | **2,163** | **-** | **989** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (17,270) | - | - | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 2,163 | (2,163) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **-** | **-** | **(15,107)** | **(2,163)** | **-** | **-** |
| **Mwaka Uliopita 2021** | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(89,329)** | **1,716** | **-** | **989** |
| Athari za urekebishaji wa makosa | - | - | - | - | - | - |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (9,557) | - | - | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (447) | 447 | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(99,334)** | **2,163** | **-** | **989** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi. Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na Ernst & Young, Certified Public Accountants (T), na kupokea taarifa huru ya uhakiki wa ukaguzi.

Taarifa hizi za fedha ziliidhinishwa na bodi ya wakurugenzi siku ya tarehe 28 April 2023

I. John
(Mkurugenzi mtendaji) — Imesainiwa tarehe 28 April 2023

Mr. P. Ishengoma
(Mkurugenzi) — Imesainiwa tarehe 28 April 2023

# DC apiga marufuku ujenzi kwenye miinuko

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, Emmanuela Kaganda, ameagiza wananchi waliojenga na wanaofanya shughuli za kilimo maeneo ya miinuko na kwenye vyanzo vya maji, kusitisha shughuli hizo.

Aidha, Kaganda ametahadharisha kuwa watakaokaidi amri hiyo halali, serikali itawaondoa kwa nguvu na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Alitoa hadhari hiyo jana katika Kata ya Olturumet, wakati akikabidhi tani 4.4 za mahindi na kilo 290 za maharage, kwa kaya 323 zilizoathirika na mvua kubwa inayoendelea na kusababisha mafuriko.

"Naagiza wananchi wote waliojenga na wanaofanya shughuli za kilimo maeneo ya miinuko, milimani na kwenye vyanzo vya maji kuacha mara moja kwa kuwa serikali itawaondoa kwa nguvu na kuwachukulia hatua kali za kisheria," alisema.

Aidha, alisema serikali inatambua madhara waliyopata wananchi na wametoa msaada huo mdogo wa chakula, lakini wako kazini kuendelea kufanya marekebisho ya miundombinu ya barabara kupitia kwa kutumia mitambo ya halmashauri hiyo.

Kadhalika, aliwataka wananchi wa eneo hilo, kuchukua tahadhari wakati mvua ikinyesha, kutunza mazingira na kuwakemea watu wote wanaoharibu mazingira kwa kuwa uharibifu huo unasababisha madhara mvua inaponyesha.

"Historia inaonyeshwa na kuthibitihshwa na wazee wa maeneo haya kuwa zamani mvua ilinyesha, lakini kutokana na uharibifu wa mazingira kwa sasa mvua ndogo inaponyesha huleta madhara makubwa sana, hivyo tunawaomba wazee kuchukua hatua ili kuzuia madhara haya yasiendelee kutokea," alisema Emmanuela.

Pia, viongozi wawakili wa wananchi wakiwamo wenyeviti wa vijiji na vitongoji na madiwani, wameishukuru serikali kupitia Ofisi ya Mkuu Wilaya hiyo, kwa msaada huo, kwa kuwa ni muhimu kwa wananchi waliopata madhara.

"Tunakushukuru Mkuu wa wilaya kwa kuwa tangu siku ya kwanza mafuriko yalipotokea, ulikuwa pamoja na sisi na umepiga hatua nyingine kwa kuwaletea wananchi hawa chakula ambacho wengi wao akiba ilichukuliwa na kuharibiwa na mvua hizo," alisema Diwani wa Olturumet, Joseph Tinayo.

Vilevile viongozi hao waliomba serikali kuweka mpango madhubuti wa kurekebisha barabara ambazo zimeharibiwa na mvua kwa kuwa nyingi hazipitiki na zinasababisha adha kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Selemani Msumi, alisema kati ya mahindi tani hizo 4.4, Benki ya NMB, Kanda ya Kaskazini, imetoa kilo 3,000 za mahindi na kilo 290 za maharage.

Wakati, serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa wilaya hiyo, imetoa kilo 1,400, madaftari 300 na kalamu 336 kwa wanafunzi 188.

Katika wilaya hiyo, kaya 543 zilipata madhara kutokana na mvua kubwa iliyonyesha usiku wa kuamkia Machi 23, mwaka 2023, na kaya 323, ndizo zilizoathirika zaidi.

Kaya hizo ziko kata za Kimnyaki, Sambasha, Olturumet na Olmotonyi.

# Vijana 130 wanufaika mradi KCB tujiajiri

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

VIJANA 130 wa Mkoa wa Kilimanjaro, wamepata mwanzo mpya na wenye matumaini, baada ya kuwezeshwa kujiajiri kupitia mradi wa KCB tujiajiri. Mradi huo maarufu 'KCB 2jiajiri' unatekelezwa na Mfuko maalum wa Benki ya KCB Foundation na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ).

Akizungumza jana, wakati wa kuwaaga wahitimu wa mafunzo hayo yaliyotolewa na Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema uwezeshaji wa vijana ni jambo muhimu katika kuchochea maendeleo ya taifa.

"Mradi huo umefadhiliwa kwa ubia wa asilimia 50 kwa 50 na Benki ya KCB, kupitia KCB Foundation na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) ili kuongeza fursa za kuajiriwa na kujiajiri kwa vijana 960.

"Uwapo wa vijana wenye ujuzi katika maeneo mbalimbali ya kimkakati, kutasaidia kufungua fursa mpya za ajira na kuongeza kipato kwa vijana nchini. "Uwezeshaji wa vijana ni muhimu katika kuchochea na kufikia malengo makubwa ya kitaifa. Tunaamini mkitoka hapa mtaweza kujiajiri na kuajiri wengine zaidi. "Uwekezaji huu uliofanywa na benki ya KCB na GIZ ni hatua kubwa kwa maendeleo ya nchi na umewezekana kutokana na mazingira rafiki ambayo serikali ya awamu ya sita imeyaweka. Tunapongea juhudi hizi na serikali tutaendelea kuwaunga mkono."

Benki ya KCB kupitia KCB Foundation, imeweka mikakati mbalimbali ya kuwezesha jamii kijamii, kielimu na kiuchumi, wanawake na vijana ni moja ya maeneo ya vipaumbele.

Awali, Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Uhusiano wa KCB, Christine Manyenye, alisema mradi huo umelenga kufungua fursa za kiuchumi kwa vijana nchini kwa kuangalia maeneo yenye uhitaji wa ajira ikiwamo sekta ya ujenzi.

"KCB tumekuwa mstari wa mbele kuhakikisha tunaboresha maisha ya Watanzania kwa kuleta suluhisho za muda mrefu kwenye changamoto mbalimbali. Tunafurahi kutekeleza mradi huu kwa mafanikio na leo hii tunatoa vitendea kazi kwa vijana waliofanya vizuri zaidi ili waweze kuanzisha biashara zao na kuajiri vijana wengine," alisema. Katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mkazi wa GIZ, Dk. Mike Falke, alisema "Tunafurahishwa na matokeo ya ushirikiano huu ambao unaendana na vipaumbele vya serikali katika kuongeza ujuzi na ajira nchini," alisema.

"GIZ tunatambua utayari wa Serikali ya Tanzania katika kuwekeza kwa vijana na GIZ-E4D pamoja na VETA tunalenga kutoa mafunzo lwa vijana 7,000 na kutoa ajira mpya 3,300 na kuwezesha kufungua biashara 100 nchini," alisema.


TEMBO NICKEL

## VACANCY

## CONSTRUCTION MANAGER

**Position Summary:**
Tembo Nickel is seeking to recruit Construction Manager to join the Tembo Nickel Project Team. This role is based at Ngara Site. The Construction Manager will be responsible for the direction and management of all construction projects through design, implementation, development, and delivery. The successful candidate for this role will report to the Mine General Manager and will work a 6/3 Roster.

**Principal Accountability**
- Ensure the whole construction Team operates in safe environment.
- Develop and lead the set-up, planning, development, implementation, and execution of construction project in terms of world's best practices.
- Direct and manage construction studies i.e., Conceptual, Scoping, Preliminary Economic Assessments (PEA), Pre-feasibility and Feasibility.
- Direct construction project's technical disciplines across the life cycle and manage internal and external stakeholders to the successful delivery of the project.
- Lead potential due diligence processes on the project with financial institutions.
- Setup construction team, complete with resources and structures which may include technical support, project controls, project management, external consultants, contractors etc.
- Direct, manage and coordinates the efforts of various project and control managers to ensure that the projects are developed and executed in accordance with respective budgets, timelines, and quality.
- Ensure that construction project contribute towards the social, economic, and institutional development of all stakeholders.
- Ensuring stringent application to safety, health, environmental and quality policies, avoid harm to people and the environment and ensure compliance with all regulatory and legal requirements.
- Optimize construction project outcomes through rigorous contract management, claim management, risk, and opportunity management.
- Direct and control the master baseline schedules for the development of any construction project.
- Manage the project budget and monitors actual spent and forecast to complete to ensure the projects does not exceed budgets.
- Makes presentations to potential investors, business partners and company executives concerning different phases and updates of the construction projects.
- Develop and implement capital projects risk management strategies.
- Has good leadership and management skills.

**Experience and Qualifications**
- The Construction Manager should be a Construction Professional with a degree in either Project Management or mechanical engineering and have relevant construction experience.
- 10-15 years of project management experience, specific to the mining, mineral processing and metals industry is compulsory.

Tembo Nickel offers a competitive remuneration package and ONLY shortlisted candidates will be contacted.

**How to Apply**
Applicants are invited to send their resumes indicating the role title in the subject via email **jobs@tembonickel.com**

**Application closing date is 19th May,2023**
Note: We are committed to provide equal employment opportunities based on merits and we do not charge candidates any fees in the whole recruitment process

**Women are strongly encouraged to apply.**

**For and on behalf of Tembo Nickel, Kabanga Nickel Project**

HABARI KITAIFA

# ‘Bunge lipitishe azimio la kuibana serikali kujitoa OGP’

**Na Romana Mallya**

WAKATI serikali ikitangaza kurejea katika Mpango wa Uendeshaji Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP), wadau wa utawala bora wamependekeza kuwe na azimio la Bunge kuzuia serikali kujitoa kwenye mpango huo.

Hoja hiyo iliibuliwa jana jijini Dar es Salaam wakati wa asasi za kiraia Tanzania zikiadhimisha wiki ya Uwazi serikalini, zikijiandaa kurejea rasmi kwa Tanzania kwenye OGP, mkutano ulioandaliwa na TWAWEZA.

Katika maadhimisho hayo, Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe (pichani), katika meza ya majadiliano kuhusu OGP na serikali za mitaa, alisema wanapenda kuishauri serikali namna watakavyoingia OGP iwe tofauti na walivyoingia mara ya mwisho.

“Angalau waziri mhusika kwa mujibu wa ile barua ilipelekwa kwa Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Wakati tunaanza ilikuwa chini ya Ofisi ya Rais. Waziri mhusika apeleke azimio bungeni ili Bunge litoe makubaliano ya Tanzania kujiunga.

Zitto alisema azimio hilo liwekwe sharti kwamba, serikali ikitaka kujitoa Bunge ndiyo liamue suala hilo.

“Hii itaongeza hatua za uamuzi, Rais kaingia ameamua, Rais mwingine ameingia ameamua uwazi unakuwa haipo, tukiongeza uamuzi kwa mfano kwa azimio la Bunge itatusaidia sana kuhakikisha kwamba tunajilinda.

“Kwa sababu OGP si jambo la ajabu, ni jambo la kawaida la uwazi na uwajibikaji vitu ambavyo ni miongoni mwa tunu za taifa. Ukisoma zile tunu kwenye ripoti ya Jaji Joseph Warioba yote yamo, uwazi uwajibikaji ushirikishwaji wakati wa Awamu ya Tatu, kaulimbiu ya Rais Hayati Benjamin Mkapa, ilikuwa ni ‘Uwazi na Ukweli’,” alisema.

Alisema mchakato wa OGP ni wa kubadilisha kutoka kwenye utamaduni wa namna gani serikali inaendeshwa kwa ushirikishwaji wa serikali yenyewe, asasi za kiraia, sekta binafsi na wananchi.

Alisema anadhani hilo ndiyo moja ya pendekezo wanalotakiwa kuishawishi serikali kutimiza dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kurudi kwenye OGP ilete bungeni kupitia azimio la bunge ili kulinda na kurefusha mchakato wa kujitoa inapotokea.

Alisema endapo wataingia kupitia bunge na kufanya shughuli za kuimarisha utamaduni wa kuendesha serikali kwa uwazi, uwajibikaji na ushiriki, itafikia hatua kuwa ni utamaduni na mtu akitaka kujitoa watu watamshangaa.

Mraghbishi Rukia Masayanyika alisema kwenye kujitoa lazima kuwe na utaratibu uliosemwa na Zitto kwa kuwa wakati Tanzania ikijitoa kamati za wananchi za OGP wakati huo zilikuwa na mipango kazi yao inaendelea.

“Lazima tuwe na mtazamo kwamba nchi ikiingia kuwe na jambo ambalo litahakikisha wakati wa kujitoa pia kuwe na tangazo maalum badala ya kunong’onezana huku watu wanatekeleza huku tunaambiwa Tanzania imejitoa,” alisema.

Hata hivyo, Masayanyika alisema OGP ilikuwa na mafanikio ndani ya muda mfupi kwa sababu ya uwazi na watu kushiriki katika kuibua masuala yao na kuyachambua kwa pamoja na kupanga mikakati ya kuleta utekelezaji.



Mkurugenzi Mtendaji wa TWAWEZA, Aidan Eyakuze, alisema asasi za kiraia na vyombo vya habari vya Tanzania vinajiandaa kuelekea hatua ya kurejea rasmi uanachama wa OGP baada ya kujiondoa mwaka 2017 ilipojiunga mwaka 2011.

Alisema katika mkutano huo washiriki wamepata fursa kukumbushana mafanikio ya safari ya Tanzania ilipokuwa mwanachama na kuangazia baadhi ya fursa wanazoweza kuzitumia baada ya kurejea tena.

Alisema mwezi Machi, mwaka huu, Rais Samia akizungumza kwa njia ya mtandao katika mkutano wa pili wa Summit for Democracy alisema: “Ningependa kuuhakikishia mkutano huu kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kusimamia demokrasia, haki za binadamu na utawala bora ndani na nje ya nchi na tunalifanyia kazi suala la Tanzania kurudi katika jumuiya ya OGP katika wakati mwafaka,” mwisho wa nukuu.

Eyakuze alitaja umuhimu wa kuingia OGP ni pamoja na kuboresha utoaji wa huduma za jamii, kulinda na kupanua uhuru wa kiraia, uwazi katika sekta ya ardhi na uchimbaji madini.

## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | 1.NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.151,KITALU 'Q10' HATI NAMBA 143195-KIBAMBA 2.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO-CHAMAZI DOVYA | AHMAD KASSIM OMARY | 1.KIBAMBA 2.CHAMAZI DOVYA | 25/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | OMARI SAIDI OMARI | NYUMBA | MIZE MASOUD HASSAN | MIKWAMBWE-KIGAMBONI | 26/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.175184 KIWANJA NA.1370 KITALU "A" | KASSIAN ANTON NINDI | TABATA KISUKULU | 23/05/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | NYUMBA | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | MBAGALA KIBURUGWA | 29/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | SEVERINI BONAVENTURA LYIMO | NYUMBA | SEVERINI BONAVENTURA LYIMO | MBEZI MTONI-MTONGANI | 26/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | ZULFA SHAFII MALENDA | NYUMBA | HALIMA SHAFII MALENDA | NZASA -CHARAMBE | 29/05/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | FAISAL SALUM HASSAN | 1.NYUMBA 2.GARI T396 DJR HINO RAINBOW | FAISAL SALUM HASSAN | 1.KIGOGO-KIGAMBONI 2.TEMEKE | 30/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ANGWA CONSTRUCTION CO. LTD | NYUMBA | JASSON ALPHONCE MWAKITWANGE | BUNJU 'A' | 30/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ALOYCE PETER NSOLEZI | NYUMBA | ALOYCE PETER NSOLEZI | GOBA | 31/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | FLORA JOHN CHUWA | NYUMBA | DAVID BENEDICT KITAU | MIKWAMBWE-KIGAMBONI | 31/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | HAMAD ABDALLA MNEMBWE | NYUMBA | HAMAD ABDALLA MNEMBWE | TANDALE | 17/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | TRAZIAS ISHENGOMA | NYUMBA | TRAZIAS ISHENGOMA | MBAGALA MWANAMTOTI | 18/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | MBAWALA ACADEMCY | NYUMBA | RAMADHANI JUMANNE MBAWALA | CHAMAZI MSUFINI | 23/05/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | MPOKI BROWN MWAIPASI | NYUMBA | MPOKI BROWN MWAIPASI | KILUVYA | 26/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | IGELEGELE BUGARIKA NA BUJINGWA-MWANZA | 24/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MANGWE EMMAUEL WAMBURA | VIWANJA VIWILI VYENYE HATI MILIKI | MANGWE EMMAUEL WAMBURA | ILALILA-MWANZA | 25/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | CHRISTOPHER MANGARAYA WAMBURA | KIWANJA | CHRISTOPHER MANGARAYA WAMBURA | BUJINGWA-MWANZA | 26/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | HAWA HATIBU MUNISI | NYUMBA | RESTUS JULIUS KIMATH | NYASAKA-MWANZA | 24/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | FRIDA FRANCIS KAJUNA | NYUMBA | FRIDA FRANCIS KAJUNA | GEITA | 26/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA | JAMES JACOB KALULEMA | MAHINA KANYERERE-MWANZA | 29/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SIKITU HAMIS YAHAYA | NYUMBA | HAJI ABEID KASUBI | NYASAKA ILEMELA MWANZA | 29/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | DICKSON ANICETH GREEN | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | DICKSON ANICETH GREEN | BUJINGWA -MWANZA | 15/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | FELISTA MATOKE NYANGWE | NYUMBA YENYE HATI NA.45634,KIWANJA NA.183 KITALU 'B' | SOPHIA KIBOKO CHACHA | KISEKE-MWANZA | 29/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | FALLACK ADAM RUTUNGO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MADADIA ALLY SANKA | MKOLANI NYAMAGANA | 25/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MTONDI SIAGI KICHELE | NYUMBA (2) MBILI ZENYE HATI MILIKI | 1. MTONDI SIAGI KICHELE 2.KURUTHUMU ABDALLAHMAN NYAMKO | 1.NYAMALANGO -MWANZA 2.NYAKATO -MWANZA | 25/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYUMBA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYASAKA ILEMELA MWANZA | 07/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | SONGALELI SAMA MZEE | NYUMBA | SONGALELI SAMA MZEE | BUSWELU MWANZA | 07/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | NOZAWA G DAVID,MR. T/A BUSWELU SATELITE CABLE NETWORK | KIWANJA | KATONGOLE DASTAN | NORTH BUSWELU-MWANZA | 18/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ARUSHA | ISIMBULA MAULID RAJABU | KIWANJA | ISIMBULA MAULID RAJABU | MURIET -ARUSHA | 18/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ARUSHA | JOHN LEONARD MAIGE | KIWANJA | JOHN LEONARD MAIGE | MURIET -ARUSHA | 18/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 18/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BRAITON RUBEN MWANKEMWA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | BRAITON RUBEN MWANKEMWA | IVUMWE -MBEYA | 16/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 19/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BARAKA PAUL DABAVUNJE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | BARAKA PAUL DABAVUNJE | UYOLE-MBEYA | 23/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 25/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 26/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 25/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 23/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | SWABRI HAMIS ISSA | NYUMBA | SWABRI HAMIS ISSA | SALASALA | 29/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | MATHAYO GABRIEL MJEMA | NYUMBA | MATHAYO GABRIEL MJEMA | MIVUMONI-WAZO | 29/05/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | EMMANUEL ALFREDY LAIZER | NYUMBA | EMMANUEL ALFRED LAIZER | MAPINGA BAGAMOYO | 30/05/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MWAJUMA SHABANI MPONDI | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA. TMK000450 | MWAJUMA SHABANI MPONDI | TOROLI - CHANG'OMBE | 24/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | YAKUB ISSA KIDUNDA | NYUMBA | YAKUB ISSA KIDUNDA | KIPUNGUNI-UKONGA | 25/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | SHABANI RASHIDI NAENJE | NYUMBA | SHABANI RASHIDI NAENJE | MLAMLEMI MKURANGA | 25/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | RASHIDI HAMADI CHALAMILA | NYUMBA | RASHIDI HAMADI CHALAMILA | MLAMLEMI MKURANGA | 25/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | DEVOTA JOHN KATINDASA | NYUMBA | MASOUD HAMAD SEIF | KICHANGANI MAJOHE | 31/05/2023 SAA 8:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MARIAM DARUWESHI IDDI | NYUMBA | MARIAM DARUWESHI IDDI | KIBUGUMO-KIGAMBONI | 08/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | JOHN JAMES MASWI | NYUMBA | JOHN JAMES MASWI | ZAVALA CHANIKA | 13/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | JUMA MOHAMEDI MASUDI | NYUMBA | JUMA MOHAMEDI MASUDI | MAKANGARAWE TEMEKE | 22/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | SADICK SEIF MWERA | NYUMBA (2) | SADICK SEIF MWERA | 1.MBONDOLE MSONGOLA 2.AZIMIO KICHANGANI | 30/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | DAVID ABEL MLAU | CHARAMBE -MBAGALA | 27/06/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| UBUNGO | DOTO HARUN MSUYA | NYUMBA | DOTO HARUN MSUYA | TANGINI-KIBAHA | 10/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ALPHANI JAFARI JUMA | NYUMBA | ALPHANI JAFARI JUMA | MIEMBE SABA -KIBAHA | 10/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | SEGUMBA JAPHAR MHANDO | NYUMBA | SEGUMBA JAPHAR MHANDO | VIWEGE MAJOHE | 23/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | SEIF HAMAD NASSORO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | SEIF HAMAD NASSORO | MBAGALA KILUNGULE | 18/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | HUSSEIN NASIBU JUMA | NYUMBA | DEVOTA FRUMENTUS MBUGA | MAILI MOJA KIBAHA | 19/05/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | YUSUPH MOHAMED ALLY | NYUMBA | YUSUPH MOHAMED ALLY | SAGULO PUGU | 26/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0715868000/0754376493/0714939933/0759648448/0759282344/0753575752/0655715138/0787129539
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA MAJI

**MUHTASARI WA BAJETI HIYO AMBAYO IMEGAWANYIKA KATIKA MAENEO MAKUU YAFUATAYO; HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI; UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2022-2023; MAFANIKIO YA MIAKA MIWILI YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA MAJI, CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA; VIPAUMBELE NA MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2023/2024; NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024.**



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akikata utepe katika hafla ya kukabidhi mitambo ya kisasa ya kuchimba visima na mitambo ya kujenga mabwawa iliyosambazwa katika kila mkoa hapa nchini.

## JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA

## WIZARA YA MAJI

**JUMATANO YA TAREHE 10 MEI, 2023, WAZIRI WA MAJI, MHE. JUMAA HAMIDU AWESO (MB), ALIWASILISHA HOTUBA YA BAJETI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA 2023/2024. UFUATAO NI MUHTASARI WA BAJETI HIYO AMBAYO IMEGAWANYIKA KATIKA MAENEO MAKUU YAFUATAYO; HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI; UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2022-2023; MAFANIKIO YA MIAKA MIWILI YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA MAJI, CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA; VIPAUMBELE NA MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2023/2024; NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024.**

**1. HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI**

1. Maelezo kuhusu hali ya Sekta ya Maji nchini kwa kuzingatia hali ya rasilimali za maji; ubora wa maji; na upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini.

**2.1 Hali ya Rasilimali za Maji**

2. Rasilimali za maji zilizopo nchini ni wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka ambapo juu ya ardhi ni mita za ujazo bilioni 105 na ardhini ni mita za ujazo bilioni 21. Hivyo, kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni wastani wa mita za ujazo 2,105. Hii ni kwa idadi ya watu milioni 59.8 waishio Tanzania Bara kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022. Kiwango hicho ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa. Hivyo nchi haijaingia kwenye uhaba wa mahitaji ya maji.

3. Takwimu zinaonesha kwamba nchi yetu inatarajiwa kufikia kiwango cha wastani wa mita za ujazo 1,700 kwa mwaka kwa mtu ifikapo mwaka 2030. Aidha, takwimu zinaonesha kwamba mahitaji ya maji nchini kwa sekta mbalimbali mwaka 2022 yalikuwa ni wastani wa mita za ujazo bilioni 62 na yanatarajiwa kufikia mita za ujazo bilioni 75 mwaka 2030. Hivyo, tunao wajibu wa kuendelea kuongeza msukumo katika utunzaji wa rasilimali za maji, kuongeza ufanisi katika matumizi ya maji pamoja na kuongeza upatikanaji wa maji ikiwa ni pamoja ujenzi wa mabwawa

.

**2.2 Hali ya Ubora wa Maji**

4. Ubora wa maji ni kigezo muhimu katika kutoa maamuzi juu ya matumizi mbalimbali ya maji. Hali ya ubora wa maji katika maziwa, mito, mabwawa, chemichemi na visima inakidhi viwango hivyo vinaweza kuendelezwa na kutumika kwa matumizi mbalimbali ya shughuli za kiuchumi, kijamii na mazingira. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuweka katika teknolojia mbalimbali za kusafisha na kutibu maji ili kuhakikisha maji yanayotumika yanafaa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**2.3 Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini**

5. Hali ya upatikanaji wa huduma za maji vijijini imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 74.5 mwezi Desemba, 2021 hadi kufikia wastani wa asilimia 77 mwezi Desemba, 2022. Kiwango hicho kimeongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji kwenye maeneo ya vijijini kufikia 30,209,409 hivi sasa

**2.4 Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini**

6. Hali ya huduma ya majisafi na salama katika maeneo ya mijini imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 86.5 mwezi Desemba, 2021 hadi wastani wa asilimia 88 mwezi Desemba, 2022. Kiwango hicho kimeongeza idadi ya wananchi 2,345,537 wa maeneo ya mijini wanaopata huduma ya maji.

7. Huduma ya uondoshaji majitaka katika maeneo ya mijini imeendelea kuimarika ambapo mtandao wa mabomba ya majitaka umeongezeka kutoka kilomita 1,385.8 mwezi Aprili 2022 hadi kufikia kilomita 1,416.93 mwezi Aprili 2023. Aidha, kwenye miji ya Geita, Kahama, Magu, Misungwi, Lindi, Kigoma, Sumbawanga, Bukoba na Lamadi ambayo haina mtandao, huduma ya uondoshaji majitaka inatolewa kwa utaratibu wa magari na mabwawa ya kutibu majitaka.

**3.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2022/23**

**3.1 Upatikanaji wa Fedha**

8. Mwaka 2022/23, Fungu 49 – Wizara ya Maji iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 709.36; kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 51.46 ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 657.89 ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Aprili 2023, Wizara imepokea jumla ya Shilingi bilioni 686.37 sawa na asilimia 96.76 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi bilioni 648.08 ni za kutekeleza miradi ya maendeleo na Shilingi bilioni 38.29 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**3.2 Programu na Miradi Mbalimbali Iliyotekelezwa katika mwaka 2022/23**

9. Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi na mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

**3.2.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

10. Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji unahusisha tathmini na ufuatiliaji wa rasilimali za maji; kuhifadhi na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji; kugawa maji kwa sekta mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji na kiasi cha maji kilichopo; na kuendeleza rasilimali za maji. Hadi mwezi Aprili 2023, vituo 136 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji vimekarabatiwa na vituo sita (6) vimejengwa; vibali vipya 1,554 vya matumizi ya maji na vibali 630 vya kuchimba visima vya maji vimetolewa; leseni 105 zimehuishwa; na vyanzo 63 vimewekewa mipaka. Vilevile, ujenzi wa mabwawa 10 ya ukubwa wa kati na madogo umekamilika na ujenzi wa mabwawa 40 unaendelea.

11. Naomba niwahimize wananchi wote wanaotaka kutumia maji kutoka katika vyanzo mbalimbali wafahamu kuwa wanao wajibu wa kisheria wa kuomba vibali vya matumizi ya maji kutoka katika Bodi za Maji za Mabonde.

**3.2.2 Huduma za Ubora wa Maji**

12. Mwaka 2022/23, Wizara ya Maji kupitia Maabara za Ubora wa Maji imeendelea kusimamia na kufuatilia ubora wa maji nchini. Vilevile, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa madawa ya kusafisha na kutibu maji pamoja na kuhakiki ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira. Jumla ya vyanzo vya maji 1,473 ambavyo ni mito, maziwa, chemichemi na mabwawa vilihakikiwa ubora wake. Matokeo ya uchunguzi yalionesha kuwa ubora wa maji wa vyanzo vya maji nchini na mitandao ya kusambaza maji ni wa kuridhisha.

13. Natoa wito kwa wadau wote kutambua umuhimu wa kupima maji kabla ya kuyatumia kwa matumizi mbalimbali.

**3.2.1 Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini**

14. Mwaka 2022/23, Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilipanga kutekeleza jumla ya miradi 1,029 ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya miradi 586 imekamilika na miradi mingine utekelezaji wake unaendelea.

15. Katika kuhakikisha miradi ya maji vijijini inakuwa endelevu, hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya vyombo 111 vya Watoa Huduma ngazi ya Jamii (CBWSOs) vimeundwa na kusajiliwa na hivyo kuwa na jumla ya CBWSO 2,515 zilizosajiliwa. CBWSOs hizo zimeajiri jumla ya wataalam 5,296 kwa ajili ya uendeshaji. Vilevile, Serikali imeendelea kuzijengea uwezo CBWSOs kwa kutoa mafunzo maalum kuhusu utunzaji, uendeshaji na usimamizi wa miradi ya maji vijijini; kununua vitendea kazi; na kujenga majengo ya ofisi.

16. Wizara ya Maji kupitia RUWASA inatekeleza Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Program for Results-P4R) ambapo fedha hutolewa kutokana na matokeo ya utendaji. Awali, Programu hii ilianza kutekelezwa katika mikoa 17 (Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Manyara, Mara, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Shinyaga, Simiyu, Singida, Songwe na Tabora). Awali Programu hiyo ilitengewa Dola Milioni 350, katika kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji wake, programu imeonesha mafanikio yaliyopelekea Benki ya Dunia kuongeza kiasi cha Dola za Marekani Milioni 300 na kufanya kuwa na jumla ya Dola Milioni 650.

17. Fedha zinazotolewa zinatokana na matokeo ya utendaji ambapo anayefanya vizuri anapata fedha nyingi zaidi. Kwa mfano Halmashauri ya Nzega ilianza kwa kupewa fedha za awali Shilingi Bilioni 1.3 mwaka 2020/21 na mwaka 2022/23 imeweza kupata Shilingi Bilioni 10.3. Kutokana na utendaji mzuri na kuongezeka kwa fedha, programu itatekelezwa katika mikoa 25. Mikoa iliyoongezeka ni Njombe, Mbeya, Morogoro, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Dodoma ambapo kwa kila Halmashauri ya Wilaya itapewa Shilingi Milioni 961 kama fedha za awali.

**3.2.2 Huduma za Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini**

18. Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza miradi ya majisafi na usafi wa mazingira katika miji mbalimbali. Katika mwaka 2022/23, jumla ya miradi 175 ilipangwa kutekelezwa ambapo hadi mwezi Aprili 2023, miradi 40 imekamilika na miradi 135 inaendelea kutekelezwa na ipo

kwenye hatua mbalimbali. Baadhi ya miradi ni kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Mbeya

19. Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa kutoa maji kutoka chanzo cha Mto Kiwira kupeleka katika Jiji la Mbeya kwa gharama ya Shilingi bilioni 117. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 66.5 hadi lita milioni 184 kwa siku na kuimarisha hali ya huduma ya maji kutoka asilimia 80 hadi asilimia 95.

(b) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Dodoma

20. Katika mpango wa muda mfupi wa kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dodoma, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Nzuguni unaogharimu Shilingi bilioni 5. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 68.7 hadi lita milioni 76.3 kwa siku na utawanufaisha wakazi wa maeneo ya Nzuguni, Ilazo, Swaswa na Kisasa.

21. Serikali inaendelea kutafuta vyanzo vya maji vya uhakika kwa ajili ya Jiji la Dodoma ikiwemo ujenzi wa Bwawa la Farkwa na kutoa maji Ziwa Victoria.

(c) Miradi ya Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya Maeneo ya Mkoa wa Pwani

22. Serikali inatekeleza miradi ya kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na miji ya Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze na Bagamoyo katika Mkoa wa Pwani. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na mradi wa ukarabati na upanuzi wa mfumo wa kusambaza majisafi ambao umekamilika na kuzinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 16 Machi, 2023; mradi wa usambazaji maji maeneo ya Mbezi – Makabe; na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji kutoka katika visima virefu vya Kimbiji na Mpera. Katika kuhakikisha maji yanapatikana kwa kipindi chote cha mwaka, Serikali imeanza ujenzi wa bwawa la Kidunda na mkandarasi yupo eneo la kazi na malipo ya awali shilingi bilioni 49 yamefanyika.

(d) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Mwanza

23. Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kusafisha na kutibu maji katika eneo la Butimba kwa gharama ya Euro 26,165,102 (sawa na shilingi bilioni 69). Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 71. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023 na utawanufaisha wakazi wa maeneo ya Jiji la Mwanza (Nyegezi, Mkolani, Buhongwa, Nyamazobe, Nyahingi, Bugando, Luchelele, Lwanima, Sahwa, Fumagila, Kishiri na Igoma); Magu (Kisesa, Bujola na Kanyama) na Wilaya ya Misungwi (Usagala, Fela, Bukumbi na Nyashishi).

(e) Mradi wa Maji Mugango – Kiabakari - Butiama

24. Serikali inatekeleza mradi wa maji Mugango – Kiabakari – Butiama kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 30.69 (sawa na shilingi bilioni 70.5). Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia asilimia 79 na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2023/24. Mradi huo utawanufaisha wakazi 100,000 waliopo katika eneo la mradi pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka bomba kuu.

(f) Simiyu Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Simiyu

25. Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi unatekelezwa kwenye Wilaya tano (5) za Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu katika Mkoa wa Simiyu. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa gharama ya Shilingi bilioni 444.6. Hadi mwezi Aprili 2023, kiasi cha Shilingi bilioni 1.97 kimetumika kulipa fidia kwa wananchi wapatao 1,364 kati ya 1,395 waliofanyiwa uthamini. Aidha, taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi zinaendelea na utekelezaji unatarajiwa kuanza katika mwaka 2023/24.

(g) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28

26. Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji huduma ya maji katika miji 28 unaogharimu Shilingi trilioni 1.48. Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi wamepatikana na wameanza maandalizi ya awali ya maeneo ya ujenzi pamoja na kukamilisha kazi ya usanifu. Miji itakayonufaika na mradi huu ni Kilwa Masoko, Nanyumbu, Makonde, Njombe, Makambako/ Wangingómbe, Ifakara, Chunya, Rujewa, Singida, Kiomboi, Manyoni, Chamwino, Chemba, Mugumu, Tarime/Rorya, Sikonge, Urambo/Kaliua, Kasulu, Mpanda, Songea, Geita, Chato, Kayanga, Mafinga, Handeni, Korogwe, Muheza na Pangani.

(h) Miradi ya Maji katika Miji mingine

27. Miradi mingine inayoendelea kutekelezwa katika baadhi ya miji ni pamoja na; Majiji ya Arusha na Tanga; Manispaa za Morogoro, Shinyanga na Mtwara/ Mikindani; na Mji wa Tunduma, Tinde na Shelui.

**4.0 MAFANIKIO YA MIAKA MIWILI YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA MAJI**

28. Katika kipindi cha miaka miwili (2021 - 2022) ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu Mpendwa, mpenda wananchi wake, mwenye dhamira njema ya kumtua mama ndoo kichwani, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mafanikio makubwa yamepatikana katika Sekta ya Maji. Mafanikio hayo ni pamoja na:-

(i) Mageuzi makubwa ya kiutendaji yaliyofanyika kwa watumishi 9,422 waliopo ambao wamechangia mafanikio makubwa ya sekta kutokana na kuwa na ari ya kazi, kujituma, weledi na kubeba maono mema ya Rais wetu ya kumtua mama ndoo kichwani.
(ii) Kukamilika kwa miradi 1,373 ya usambazaji maji inayotoa huduma katika vijiji 2,649 na kufikisha jumla ya vijiji 9,737 vinavyopata huduma ya maji nchini;
(iii) Kukamilika kwa miradi 80 ya usambazaji maji mijini ambayo inatoa huduma kwa wananchi 4,305,801;
(iv) Kukwamuliwa kwa miradi 157 kati ya 177 ya maji vijijini iliyokuwa na changamoto kwa muda mrefu;
(v) Kuanzishwa kwa mfumo wa takwimu za miradi (MajiApp) na mfumo wa usimamizi wa ankara za maji (Unified billing system);
(vi) Kuongezeka kwa maabara za ubora wa maji zenye hadhi ya Ithibati kutoka maabara moja (1) ya Mwanza iliyokuwepo mwaka 2021 hadi kufikia maabara saba (7). Maabara hizo ni Singida, Shinyanga, Kigoma, Bukoba, Musoma na Dar es Salaam;
(vii) Kuanza kwa ujenzi wa mabwawa ya Kidunda na Farkwa;
(viii) Kununuliwa na kuanza kutumika kwa seti 25 za mitambo ya kuchimba visima na seti tano (5) za mitambo ya ujenzi wa mabwawa;
(ix) Kuzinduliwa kwa Mpango wa Uhifadhi wa Vidakio vya Maji nchini wa mwaka 2021 hadi 2035. Kupitia Mpango huo, jumla ya miti rafiki ya maji 2,541,803 imepandwa kwenye maeneo ya vyanzo vya maji katika mabonde yote tisa nchini; na
(x) Kufanyika kwa Marekebisho Na. 8 ya Mwaka 2022 ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 ili kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini.

29. Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama imeimarika kwa wananchi wa vijijini kutoka wastani wa asilimia 70.1 mwaka 2020 hadi asilimia 77 mwezi Desemba, 2022; na kwa maeneo ya mijini kutoka wastani wa asilimia 84 mwaka 2020 hadi wastani wa asilimia 88 mwezi Desemba, 2022.

**5.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA**

30. Changamoto kubwa zinazoikabili sekta ya maji ni:-
a) Mahitaji makubwa ya fedha za uwekezaji kwenye miradi mikubwa ya maji hasa ya kimkakati;
b) Uharibifu wa vyanzo vya maji unaotokana na uvamizi na uchafuzi; na
c) Mabadiliko ya tabianchi.

31. Katika kukabiliana na changamoto hizo, hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa zikiwemo kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya maji; kushirikiana na wadau katika kuendeleza uhifadhi na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji; kutekeleza miradi ya maji ambayo itatumia vyanzo vya maji vya uhakika kama vile mito mikubwa na maziwa; ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhi maji; na kutekeleza mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**6.0 VIPAUMBELE NA MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2023/24**

32. Mwaka 2023/24, Serikali imepanga kuwa na vipaumbele vifuatavyo:-
a) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002;
b) Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji;
c) Kuwa na mtandao wa taifa wa maji (National Water Grid);
d) Kuwa na Mpango Kabambe wa Usambazaji Maji (Water Supply Masterplan);
e) Kuimarisha usimamizi wa ubora wa maji;
f) Kukamilisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi inayoendelea na kukabiliana na upotevu wa maji (Non Revenue Water - NRW);
g) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ili kuwa na huduma endelevu ya upatikanaji wa maji;
h) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa miji 28;
i) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya usafi wa mazingira;
j) Kuendelea na ujenzi wa mabwawa madogo, yenye ukubwa wa kati na makubwa yakiwemo Kidunda na Farkwa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;
k) Kuimarisha taasisi za Wizara ya Maji ikiwemo Chuo cha Maji, Mfuko wa Taifa wa Maji na RUWASA; na
l) Kuimarisha ushirikiano na ushirikishwaji wa wadau wa sekta ya maji.

**7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024**

33. Ninaomba sasa kutoa hoja Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 756,205,106,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2023/24. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni Shilingi 60,375,474,000 ambapo Shilingi 18,035,561,000 ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 42,339,913,000 ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE). Jumla ya bajeti ya maendeleo ni Shilingi 695,829,632,000 ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi 407,064,860,000 ni fedha za ndani na Shilingi 288,764,772,000 ni fedha za nje.

Bajeti inapatikana katika Tovuti ya Wizara ya Maji, yenye kikoa cha **www.maji.go.tz**

UCHUMI

# Mikopo halmashauri yageuka mzigo wa mabilioni serikalini, badala mtaji wa umma

**Na Gwamaka Alipipi**

KUTOKUWAPO ufuatiliaji wa karibu na ukusanya marejesho ya mikopo kutoka kwenye vikundi, imo katika sababu zinazoziingiza halmashauri nchini kwenye kashfa ya kupoteza mabilioni ya pesa.

Ni kashfa inayoendana na udhibiti duni wa mikopo, kutoshirikishwa wataalamu wa mikopo kuanzia utoaji, hadi urejeshaji; fedha itokanayo na asilimia 10 za bajeti ya halmashauri kukopeshwa kinamama na vijana.

Serikali imeshatangaza kusimamishwa utoaji mikopo hiyo, ikitafuta namna bora kuyasaidia makundi, pamoja na kuzuia upotevu wa pesa, wadau wakipendekeza elimu ya ujasiriamali kwa vikundi vitakavyonufaika, kabla ya kupewa fedha hizo.

Pia, inapendekezwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, ibuni udhibiti bora katika kurejesha mikopo kwa kuhusisha wataalamu wa usimamizi mikopo, watakaohimiza uzingatiaji kurejesha mikopo kwa hiari, ili kuwapo makuzi endelevu ya mfuko.



Hafla mojawapo kuzindua mikopi ya vijana, kwenye Manipaa ya Ubungo. **PICHA: MTANDAO**

**JICHO LA KITAALAMU**

Upekuzi wa Nipashe umebaini halmashauri za mkoa Dar es Salaam, zimo katika orodha 'hali si shwari', marejeo ni tovuti ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, ikimnukuu Mkurugenzi wake, Hanifa Hamza, kwamba tangu mwaka 2017/18 walipoanza kutoa mikopo hadi Juni mwaka jana, walikopesha Sh. bilioni 18.8 kwa vikundi 5,007 na hadi sasa, Sh. bilioni saba pekee ndio zimerejeshwa.

Mkurugenzi Hanifa anaeleza kuna Sh.bilioni 11.5 kutoka vikundi 1,911 hazijafanyiwa marejesho, mkurugenzi huyo akitaja kiasi cha shilingi bilioni 2.9 deni lake limevuka muda wa marejesho.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), ya mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12 mwaka jana, akabaini mabilioni ya shilingi yako hatarini kupotea kwa kukosa udhibiti kupitia mikopo inayotolewa na halmashauri kwa makundi maalum.

CAG Charles Kichere, anabainisha kuwapo halmashauri 155 hazikukusanya Sh. bilioni 47.01 za marejesho ya mikopo kwa makundi hayo.

Kuanzia anakoishia CAG, mtazamo wa wataaalamu kutokana na ripoti hiyo ya kiserikali, Dk. Donath Olomi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi na Maendeleo ya Ujasiriamali (IMED), anaishauri serikali itafute namna ya kuwabana wanasiasa wasizitumie pesa hizo kwa maslahi binafsi.

Hapo ananyooshea kidole baadhi yao, hasa katika ngazi ya wilaya na halmamsauri, akidai wanashawishi pesa hizo zitolewe kwa baadhi ya vikundi, kwa nia ya kuvutia kura zao, hasa madiwani.

"Yule anayepewa zile pesa, anaona hakuna umuhimu wa kuzirudisha kwa sababu aliyempa ameshamwambia sababu ni ampigie kura na yeye kura, akishampigia anahesabu kama ameshamlipa, sasa nguvu ya kumdai mtu kama huyo inatoka wapi?" anahoji Dk. Olomi.

Mtaaluma Dk. Godbertha Kinyondo, anasema tatizo ni la watumishi serikailini kukosa elimu ya mikopo na fedha, hali inayokwamisha umakini kwenye utoaji na ufuatiliaji wake; akishauri serikali ishirikiane na sekta binafsi zenye ujuzi wa fedha, ikitimiza jukumu hilo kwa makubaliano maalum, kuepuka hasara.

**WAKOPAJI WAELEZA**

Mnufaika, Alex Joseph wa Dar es Salaam, anaiambia Nipashe kwamba, uhakiki wa vikundi vyao walivyombea mikopo haukufanyika, kabla ya mikopo kutolewa, kwa sababu ya kukosekana mtaalamu wa kazi hiyo.

Hapo anaungwa mkono na Richard Daniel, anayeendesha bodaboda aliyonunua kutokana na mkopo kwenye halmashauri ya mkoani Dar es Salaam, akifafanua wanakosa usaidizi kisheria na bima za mikopo ndani ya halmashauri, akinyooshea kidole mahsusi vijana, ambao ni wanunuzi wakuu wa pikipiki na bajaji.

Diwani wa Kata ya Hananasif, Manispaa ya Kinondoni, Wilfred Nyamwija, anaieleza Nipashe akiwa na dai mikopo imegubikwa na upendeleo ya kiasi cha fedha kinachotolewa, baadhi ya kata zikipewa zaidi, akitoa mfano wa kata mbili ambako wanaishi anaowataja 'wazito' watoa uamuzi wanapata zaidi.

"Sisi ndiyo wenyeviti wa kamati ya maendeleo za kata, lakini kwenye mchakato wa kuchujwa majina ya vikundi vilivyopata na vilivyokosa hatushirikishwi," anasema na kutumia mifano:

"Kikundi cha watu watano wanapewa mkopo wa shilingi milioni 10 watafanya nini? Ndiyo maana mtu anakopa anaenda kununua makochi, anakwenda kulipa kodi atarudishaje?"

Nyamwija anasema, chanzo kikuu cha fedha hizo kutorejeshwa ni wananchi hawana elimu, pia hawana miradi, wanachokifanya ni kujiunga na kisha wanamtumia mmoja wao mwenye mradi kwenda kukopa fedha na bada kugawana, kila mmoja anaelekeza katika matumizi binafsi.

> **"Sisi ndiyo wenyeviti wa kamati ya maendeleo za kata, lakini kwenye mchakato wa kuchujwa majina ya vikundi vilivyopata na vilivyokosa hatushirikishwi.**

**HISTORIA YA MIKOPO**

Inaporejewa historia ya mikopo, mwaka 1993 serikali kupitia Bunge ilianzisha Mfuko wa Fedha wa Maendeleo kwa Wanawake na Vijana, kuwainua wanawake na vijana wasiojiweza kiuchumi, wengi wasiokidhi vigezo vya mikopo inayotolewa na taasisi za fedha, kwa kukosa dhamana.

Wakati huo mikopo hiyo ilitolewa asilimia tano kwa wanawake na asilimia tano kwa vijana, hadi mwaka 2019, serikali ikarekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, kwa kuongeza kifungu mahusus kinachowezesha mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Sheria inazitaka halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa mikopo na riba, kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyosajiliwa, zikitakiwa mamlaka zote za serikali za mitaa, kutenga asilimia hizo za mapato yake, kukopesha vikundi vilivyosajiliwa.

Madhumuni yakitajwa ni kuongeza uwezeshaji kiuchumi wa vikundi tajwa kiuchumi, hata kuboresha kiwango cha maisha ya walengwa.

# Zahanati yajengwa miaka 13 bila ya kukamilika

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, ameagiza Manispaa ya Shinyanga kuhakikisha katika bajeti ya mwaka wa fedha ujao 2023/24, zinatengwa fedha kwa ajili ya kukamilisha Zahanati ya Kolandoto iliyopo katika Kijiji cha Mwamagunguli, ambayo imeshindwa kukamilika kwa zaidi ya miaka 13 sasa.

Ujenzi wa zahanati hiyo ulianza mwaka 2010 bila kukamilika huku viongozi mbalimbali wakifika kila mwaka kwenye na kuahidi kuikamilisha, lakini hakuna utekelezaji.

Samizi alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wananchi wa kata hiyo kwenye mkutano wa hadhara, baada ya kumaliza ziara ya kutembelea ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta ya elimu pamoja na afya.

Alisema kilio cha wananchi kuhusu ujenzi wa zahanati hiyo kuchukua muda mrefu amekisikia, amemuagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga kuitengea fedha na kuikamilisha ili kuwaondolea adha ya kufuata huduma za matibabu umbali mrefu.

Aidha, Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Jomaary Satura, alisema amepokea maagizo hayo na kuahidi katika mwaka wa fedha ujao, wataitengea bajeti na kuikamilisha zahanati hiyo na kisha kuanza kutoa huduma za matibabu kwa wananchi.

Baadhi ya wananchi wa eneo hilo, walisema ujenzi wa zahanati hiyo umechukua muda mrefu tangu 2010 na wamekuwa wakipata shida ya matibabu hasa kwa wajawazito na watoto kutokana na kufuata huduma hiyo umbali mrefu huku wakitegemea kukamilika kwa zahanati hiyo kuwa mwarubaini wa tatizo hilo.





Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba, (wa tatu kushoto), akikagua soko la vitunguu la Misuna, Manispaa ya Singida jana. Kushoto kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Mlagiri. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Serukamba ataka uhalali ushuru wauza vitunguu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani hapo kuchunguza uhalali wa fedha wanazotozwa wafanyabiashara wa soko la vitunguu Misuna, Manispaa ya Singida.

Serukamba aliyasema hayo alipotembelea soko hilo na kusikiliza kero za wafanyabiashara wengi wakilalamikia kutozwa Sh. 200 kwa kila gunia la vitunguu, kila wiki washusha mizigo hutoa 5,000, kila gari likingia sokoni hapo linachajiwa Sh. 10,000 na madalali kutoa 2,000, lakini fedha zote hizo hakuna stakabadhi inayotolewa.

Serukamba alisema utaratibu ni kila fedha inayotolewa lazima mtoaji apewe risiti vinginevyo vinapotelea kwenye mifuko ya watu na kuwaagiza TAKUKURU kuchunguza kama kuna jinai wawachukulie hatua za kisheria.

Aihda, amepiga marufuku wafanyabiashara kutozwa ushuru mara mbili ndani ya mkoa mmoja na kuwataka Wakuu wa wilaya kulisimamia kwa kuwa watakaoumia zaidi ni wakulima.

Marufuku hiyo imetokana na malalamiko ya wafanyabiashara kulalamikia mageti ya Manyoni na Kintinku wakidai kupoteza muda mrefu wa ukaguzi ambao unafanyika sokoni.

Serukamba alisema atawasiliana na mamlaka husika ili kuhakikisha nchi nzima wanakuwa na kipimo cha gunia la vitunguu unaofanafa ili kuleta ushindani sawa.

"Haiwezekani Singida tunajaza gunia kwa vipimo vya serikali na tunapinga lumbesa, lakini maeneo mengine wanaachwa hii haileti ushindani sokoni," alisema.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara kufuata sheria, kanuni na taratibu katika biashara zao ili kuondoa changamoto ambazo zinawakabili maeneo mbalimbali.

Malalamiko mengine ni ukosefu wa miundombinu ya soko kama uzio, uchafu kutozolewa kwa wakati hivyo kusababisha harufu kali na kukosekana vijana au vizuizi vya mvua au jua jambo ambolo Mkuu wa Mkoa alimuagiza Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa, Jeshi Lupembe kuanza kufunika eneo hilo kwa awamu na ianze kabla ya mwezi Julai.

# Wananchi watakiwa kuchangamkia fursa ununuzi wa umma

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), imewataka wananchi kuchangamkia fursa zinazopatikana katika sheria ya ununuzi wa umma ili kunufaika na kutokomeza umaskini nchini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Meneja Uhusiano kwa Umma PPRA, Zawadi Msalla, alisema, licha ya serikali kuwa na mfumo rahisi wa kuweza kufanya biashara na wazabuni kwa kufuata misingi ya haki na sheria lakini jamii imeonekana bado kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya fursa hizo.

"Watu wengi wanaonekana kutokuwa na uelewa juu ya urahisi wa kupata zabuni za serikali, ndio maana baadhi yao wanaishia kulalamikia kwa kudhani kuwa serikali inapendelea upande fulani, jambo ambalo sio kweli," alisema.

"Kupitia mfumo wa ununuzi kwa njia ya mtandao, serikali hutangaza zabuni mbalimbali kwa kuzingatia misingi ya haki, ushindani na uwazi, mpaka sasa tangu kuanzishwa mfumo huo ni wazabuni 30,200 pekee ndio waliojisajili katika mfumo huu ili kupata zabuni za serikali," alisema.

Alisema idadi inayoonekana kuwa ni ndogo zaidi kuliko ya wazabuni waliopo, suala linalosababisha kujirudia kwa wazabuni wale wale mara kwa mara kila zinapotangazwa.

Alisema fursa zenye ushindani wa kimataifa huwapa upendeleo zaidi wazabuni wa ndani ya nchi wanaotaka kufanya biashara na serikali kwa kuwapa upendeleo wa asilimia kumi zaidi dhidi ya wageni, huku biashara ya bidhaa za ndani zikipewa upendeleo wa hadi asilimia 15 dhidi ya bidhaa zitokazo nje ya nchi.

"Zaidi ya asilimia 70 ya bajeti ya serikali huenda katika ununuzi, kwa kuzingatia hilo ni jukumu la PPRA kuhakikisha ununuzi wote unaofanyika iwe ni wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma unazingatia miiko ya ununuzi," alisema.

# Watoto 11,000 huzaliwa na selimundu kila mwaka

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WATOTO 11,000 kila mwaka huzaliwa hapa nchini na ugonjwa wa selimundu, huku idadi hiyo wanaozaliwa na tatizo hilo wanakuwa hatarini kupoteza maisha kabla ya kufikisha umri wa miaka mitano.

Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, alitoa kauli hiyo kwenye uzinduzi wa upandikizaji uloto kwa wagonjwa wenye tatizo la selimundu katika hospitali hiyo.

Dk. Chandika alisema ni tatizo kubwa, lakini hivi sasa linakwenda kupata suluhisho baada ya huduma ya upandikizaji uloto kuanza kutolewa kwa wananchi katika hospitali hiyo kupitia madaktari bingwa waliobobea kwenye fani hiyo.

"Tunaona idadi hiyo ya wagonjwa wanaozaliwa na tatizo hilo ni kubwa, tunaamini hivi sasa inakwenda kupungua kwasababu tiba tayari inapatikana hapa nchini kwenye hospitali zetu," alisema Dk. Chandika.

Alisema mpaka sasa wameshapandikiza wagonjwa watoto watatu ambao wote wanaendelea vizuri na matibabu.

Akizungumzia huduma hiyo, Dk. Chandika alisema Tanzania sasa ni nchi ya kwanza kwa Afrika Mashariki kutoa huduma hiyo na ni ya saba barani Afrika, kwao ni fahari kuoa namna sekta ya afya inavyopiga hatua katika utoaji huduma kwa wagonjwa.

Alizitaja nchi nyingine ambazo zinatoa huduma hiyo ni pamoja na Algeria, Morocco, Misri, Tuniasia, Afrika Kusini, Nigeria na Tanzania ambayo tayari inatoa huduma hiyo.





# Vijana wajipanga kumweleza RC kero watumishi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

VIJANA wa Mkoa wa Mbeya, wamejipanga kwenda kwa mkuu wa mkoa huo Juma Homera, kumueleza masuala mbalimbali ya maendeleo pamoja namna bora ya kushughulika na watumishi wasiokuwa waadilifu.

Vijana hao wamefikia uamuzi huo baada ya kuona baadhi ya viongozi hawatekelezi ipasavyo majukumu yao na kusababisha wananchi kukosa huduma muhimu katika sekta ya maji, elimu, miundombinu ya barabara, afya na kilimo.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi UVCCM, Yasin Ngonyani, alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na Nipashe baada ya kuhitimishwa kwa mdahalo wa ushiriki wa vijana kwenye demokrasia na maridhiano.

Mdahalo huo ambao uliandaliwa na Shirika la Empower Youth Prosperity (EYP) kwa kushirikiana na asasi 10 zilizo chini ya mwamvuli wa You-Lead Tanzania kwa ufadhili wa Marekani nchini, uliwahusisha vijana wa kada mbalimbali mkoani hapa ambao kwa pamoja walijadili namna wanaweza kushiriki kukuza demokrasia na maridhiano kwa ustawi na maendeleo ya taifa.

Alisema kuonana na Mkuu wa mkoa, kutawapa fursa ya kujadili ajenda mbalimbali za vijana ikiwamo namna bora ya kujikwamua kiuchumi kupitia fursa zilizopo, lakini pia kuonyesha maeneo ambayo yanakasoro ili yaboreshwe kwa maslahi mapana ya mkoa.

"Katika hotuba yake alipofungua mdahalo huu wa vijana na demokrasia, Homera ametoa nafasi kwa sisi vijana kukaa naye meza moja kujadili mambo mbalimbali, kumpa ushauri ili mkoa wetu kupiga hatua kwenye maendeleo, nafasi hii kwetu ni adhimu hivyo tutaitumia ipasavyo tumejipanga tutakwenda alisema Ngonyani.

Alisema miongoni mwa maeneo watakayogusia ni uwajibikaji, wakiwa sehemu ya jamii wanashuhudia mambo mengi yanayofanywa na baadhi ya watumishi ambayo yana lengo la kukwamisha jitihada za serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi. Mkurugenzi wa Shirika la Himso, Fadhili Mtanga, aliwashauri vijana kutumia fursa zilizopo ikiwamo kilimo hususani cha umwagiliaji, ufugaji ili kujipatia kipato.

Aidha aliwashauri kuenzi falsafa za Hayati Mwalimu Julius Nyerere kuwa wazalendo kulisemea vyema taifa ili kutowapa nafasi wasiolitakia mema taifa.



Mmoja wa wakulima washiriki kutoka kijiji cha Matembo, wilayani Iringa, George Mahali (kulia), akitoa maelezo kwa wageni kuhusu utekelezaji wa programu ya bustani misitu inayotekelezwa na Shirika la Trees for the future kwa kushirikiana na Taasisi ya Clinton Development Initiative (CDI), juzi. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA.**

# Hospitali Mbeya yatunukiwa cheti cha Ithibati

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Mbeya (MZRH), imetunukiwa cheti cha Ithibati baada ya kutoa programu ya Mafunzo ya Ushirika na ya Uanachama kwa madaktari wa upasuaji na kukidhi matakwa yaliyowekwa na Baraza la Chuo cha College of Surgeons East, Central and Southern Africa (COSECSA), chenye makao makuu yake jijini Arusha.

Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji, alipokea Ithibati hiyo jana.

Alisema hospitali hiyo kwa kushirikiana na wadau waliongeza wataalamu bingwa wa upasuaji na kutoa mafunzo ya vitendo kwa watumishi ili kuongeza ufanisi.

"Hospitali yetu ina mchango mkubwa katika kutoa huduma za matibabu ndani na nje ya nchi na pia baadhi ya wataalam wanatoka mataifa mengine, lakini pia natoa wito kwa madaktari ambao wanahitaji kujiendeleza kielimu kusoma hospitalini hapo ili kuongeza ujuzi utakaowasaidia kuwa wabobezi," alisema Dk. Mbwanji.

Daktari Bingwa wa magonjwa ya ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu, hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Boniface Kivevele, ambaye amenufaika na mafunzo ya programu hiyo, alisema yatamsaidia kufanya kazi mahali popote kama Daktari Bingwa wa upasuaji.

"Mafunzo haya yamenisaidia kuongeza ujuzi kwenye utekelezaji wa majukumu yangu kwa sasa nimekuwa mbombezi na matumaini yangu ni kuwa daktari bingwa ambaye nitasifika kwa utoaji mzuri wa huduma za magonjwa ya ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu kwa nchi yangu na nje ya nchi pia," alisema Dk. Kivevele.

# Wananchi wapongezwa kukabiliana uharibifu mazingira

**Na Grace Mwakalinga,**
CHUNYA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, Bosco Mwanginde, amewapongeza wananchi wa wilaya hiyo kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za kukabiliana na uharibifu wa mazingira ambao umekuwa tishio.

Mwanginde alitoa kauli hiyo juzi alipozungumza na wananchi wa Kambikatoto kuwa jitihada hizo zimezaa matunda kutokana na wimbi la wanaokata miti ovyo, kuchoma mkaa, limeanza kupungua na wanaendelea na marufuku hiyo.

"Tunaendelea na operesheni ya kuwakamata wale wote wanaohusika na uharibifu wa mazingira naamini hatua hii itasaidia sana kuokoa uoto wa asili ambao ulipotea kutokana na shughuli za kibinadamu, na zoezi la uchomaji matanuri haya ni jitihada zetu," alisema Mwanginde.

Aidha, aliwataka wananchi kuacha mara moja shughuli za uchomaji wa mkaa ndani wilayani humo bila kuwa na kibali kutoka kwenye mamlaka zinazohusika na usimamizi wa mazingira.

Aliwataka viongozi wa wilaya kushirikiana kuhakikisha wanasimamia kuokoa ikolojia na uoto wa asili ambao kwa kiasi kikubwa umeharibiwa na wananchi ambao ni watumiaji wa nishati ya kuni na mkaa.

Katika kuhakikisha suala hilo linafanikiwa, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, aliwahimiza viongozi wa vijiji na vitongoji kusimamia sheria ndogo za kuwaadhibu wananchi wanaobainika kuharibu mazingira.

Aliwataka viongozi hao bila kujali mahusiano yao kwenye jamii kuwashughulikia kwa mujibu wa sheria hizo wanaoharibu kwa madai kuwa kufanya hivyo itasaidia kujenga hofu na kuachana na tabia ya kukata miti hovyo.



# Serikali yanufaika mgawo fedha misaada WB

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inanufaika na mgawo wa fedha za misaada ya sekta ya kibajeti kwa kupata asilimia 4.5 kutoka taasisi za kifedha za kimataifa ikiwamo Benki ya Dunia (WB).

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Ali Suleiman Ameir, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi Bakari Hamad Bakari wa Jimbo la Wawi, aliyetaka kujua Zanzibar inanufaika vipi na fedha za mgawo zinazotolewa na washiriki wa maendeleo ikiwamo taasisi za kifedha za kimataifa.

Ameir alisema, baadhi ya miradi ambayo Zanzibar inanufaika katika mgawo wake ni pamoja na utekelezaji wa Mradi wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) pamoja na Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Takwimu awamu ya kwanza (TSMP) na awamu ya pili unaotekelezwa na Benki ya Dunia.

Aliutaja mradi mwingine unaotarajiwa kutekelezwa na Benki ya Dunia hivi karibuni ni wa afya ya mama na mtoto ambao umelenga kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

Aliitaja miradi mingine ambayo Zanzibar imenufaika kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mkopo kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Zanzibar ilipata mgao wa Sh. bilioni 230 kutoka Shilingi trilioni tatu.

Alisema fedha za mradi huo kwa ajili ya unafuu wa kupambana na ugonjwa wa UVIKO -19 tayari zimetumiwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo katika sekta ya elimu ya ujenzi wa shule za ghorofa pamoja na hospitali 11 za wilaya ya Unguja na Pemba.

Aidha, Ameir aliutaja msaada mwingine ambao Zanzibar hivi karibuni imefaidika ni wa ujenzi wa jengo la abiria la uwanja wa ndege wa Pemba ambao ni miongoni mwa miradi ya kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kisiwa cha Pemba katika sekta ya usafirishaji.

Alisema Serikali ya Zanzibar imekuwa makini katika matumizi ya fedha za misaada pamoja na mikopo kwa ajili ya kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo na kiuchumi kwa wananchi wa Zanzibar.

"Zanzibar inaendelea kunufaika na mgawo wa asilimia 4.5 katika misaada ya kibajeti GBS ambao unatokana na makubaliano yaliyofikiwa na pande zote mbili," alisema.



Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi akisalimiana na Balozi wa Norway Tanzania, Elizabeth Jacobsen, alipofika Ikulu jijini Zanzibar jana, kwa mazungumzo na kumuaga baada ya kumaliza muda wake wa kazi nchini. **PICHA: IKULU**

# Minara 752 yajengwa kuimarisha mawasiliano

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, imesema jumla ya minara mipya 752 imejengwa kupitia Mamlaka ya Mawasiliano kwa wote (UCSA) hatua itakayosaidia kuimarisha mawasiliano na kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi na uwekezaji.

Hayo yalisemwa na Naibu waziri wa wizara hiyo, Nadir Abdulatif Yussuf, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Pandani, Professa Omar Fakih Hamadi, aliyetaka kujua hatua zinazochukuliwa na serikali kufikisha huduma za mawasiliano hadi vijijini zikoje kwa sasa.

Yussuf alisema hizo ni sehemu ya juhudi ya mikakati ya kuona huduma za mawasiliano zinawafikia watu wote na kuleta mageuzi makubwa ya fursa ya kiuchumi.

Alisema, Unguja mafanikio makubwa yamefikiwa katika huduma za upatikanaji wa mawasiliano na kufikia asilimia 98.

Aidha, Pemba alisema tayari huduma za mawasiliano ikiwamo za simu yamefikia kwa asilimia 90.7 huku juhudi nyingine zaidi zikifanywa kufikiwa maeneo yote. Alisema kutokana na ukaguzi uliofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), umebaini zipo changamoto katika baadhi ya shehia wananchi wake hawapati huduma za mawasiliano ikiwamo ya simu.

Alisema juhudi zimeanza kuchukuliwa kuona huduma za mawasiliano zinafika katika maeneo wanayoishi wananchi katika visiwa vidogo vya Unguja na Pemba.

Pia, visiwa vinane kati ya 26 vinakabiliwa na changamoto mbalimbali za kukosekana kwa huduma za mawasiliano ikiwamo ya simu.

Kadhalika, visiwa viwili kati ya 18 Unguja vinakabiliwa na changamoto za kukosa mawasiliano ikiwamo huduma za simu kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo wakiwamo wawekezaji.

Naye Waziri wa Ujenzi wa Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, hivi karibuni anatarajiwa kushuhudia utiaji saini wa ujenzi wa minara ya mawasiliano ya simu unaotarajiwa kufanywa kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote (UCSA).

# Baraza laambiwa taarifa ripoti ya kikosi kazi ziko tayari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, amesema ripoti ya kikosi kazi tayari taarifa zake zipo serikalini na imeundwa kamati kwa ajili ya kuyafanyia kazi mambo yote muhimu ya msingi yaliyojitokeza kwa lengo la kujenga mustakabali wa amani na utulivu.

Juma alisema hayo wakati akijibu hoja za wajumbe na kutoa ufafanuzi wa michango iliyochangiwa na wajumbe wa Baraza hilo, waliochangia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

Alisema Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ameunda kikosi kazi kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi changamoto zote zilizopo zinazohusu hali ya siasa na mustakabali wake kwa lengo la kujenga mazingira mazuri ya kisiasa.

Aliwataka wanasiasa nchini kujenga tabia ya kuvumiliana kisiasa na kuona juhudi zinazochukuliwa na serikali ya Zanzibar katika mustakabali wa kiasiasa na kuimarisha demokrasia.

"Ripoti ya kikosi kazi inafanyiwa mapitio ambapo imeundwa kamati maalumu kuyapitia mapendekezo yote na kufanyiwa kazi kwa lengo la kujenga mustabali mzuri wa kisiasa pamoja na kufanyika siasa za kiungwana," alisema.

Waziri Juma aliwapongeza wanasiasa kwa kutekeleza kwa dhati maridhiano ya kisiasa ambayo lengo lake kubwa ni kujenga mazingira ya kisiasa na kuondokana na siasa za chuki na uhasama.

Aliwataka wanasiasa kuyalinda maridhiano hayo ambayo yamefungua milango katika sekta mbalimbali ikiwamo uwekezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati kuwekezwa nchini.

"Huu ni wakati wa kuyalinda maridhiano ya kisiasa yaliyofikiwa ambayo yameonesha mafanikio makubwa ikiwamo kuimarika kwa amani na utulivu nchini," alisema.

Juma alisema serikali imetenga Shilingi bilioni nne kwa ajili ya kufanya maboresho makubwa ya jengo la Baraza la Wawakilishi Chukwani ili kukidhi mahitaji ya wajumbe pamoja na kazi zao.

Alisema kazi ya maboresho ya jengo hilo kwa ajili ya kukidhi mahitaji na matumizi ya wajumbe inatarajiwa kufanywa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023-2024.

Alisema baadhi ya mawaziri muhimu wanahitaji kuwa na ofisi katika jengo hilo pamoja na Mwanasheria Mkuu.

"Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilione nne kwa ajili ya maboresho ya jengo la Baraza la Wawakilishi ili liweze kutoa huduma zaidi kwa watendaji ikiwamo mawaziri... wapo watendaji ikiwamo Mwanasheria Mkuu au Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili, Uratibu wa Baraza hadi sasa hana ofisi," alisema.

# ACT yalia bajeti ya maji

**Na Halfan Chusi**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimeeleza kuwa bajeti ndogo ya kushughulikia upatikanji wa uhakika wa maji ni mtego wa umasikini kwa watanzania.

Hivyo, kimeitaka serikali kuongeza bajeti ya miradi ya maendeleo ili kutanua mitandao ya maji kwenda vijijini zaidi na kuwaondoa watanzania katika mtego huo ikiwa ni pamoja na kuanzisha gridi ya taifa ya maji kwa lengo la kuongeza kasi ya usambazaji maji.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ester Thomas, Waziri Kivuli wa Maji na Mazingira wa chama hicho kupitia hotuba mbadala ya wizara hiyo.

Alisema mwenendo wa upatikanaji wa maji vijijini upo nyuma ya malengo ya muda wa kati - kwamba kufikia mwaka 2020, asilimia 80 ya wananchi vijijini watapata huduma ya maji na 2022 malengo hayo yamefikiwa kwa asilimia 77 pekee.

"Changamoto ya upatikanaji wa maji inachangia sana kuwashikilia watu wa vijijini kwenye dimbwi la umasikini, gharama za maji wanazotumia wananchi ili waweze kuishi ni kubwa mno maeneo ya vijijini kiasi kwamba zinazidi wastani wa pato la mtu mmoja kwa siku nchini," alisema.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Uchumi wa Taifa ya Juni 2021, "Pato la Taifa mwaka 2020 lilikuwa Sh. trilioni 148.5, huku idadi ya watu Tanzania Bara ikikadiriwa kuwa watu milioni 55.9 mwaka 2016, sawa na wastani wa kila mtu kuwa na Sh. 2,653,790.

Alitolea mfano wa kipato hicho kwa Kijiji cha Gehandu huko Mbulu mkoani Manyara ambako mwananchi ananunua maji pipa moja la lita 200 kwa Sh. 7,000 huku familia moja ikihitaji angalau pipa moja kwa siku kwa matumizi ya kujibana - kwamba atatumia Sh. milioni 2.5 kwa mwaka kununua maji.

# CHADEMA yafafanua kauli ya Lissu kuhusu maridhiano

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mrema, ametoa ufafanuzi kuhusu kauli ya Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Tanzania Bara, Tundu Lissu, kuhusu maridhiano yao na serikali.

Amebainisha kuwa kati ya mambo 12 waliyokubaliana katika mazungumzo yao na serikali, hawakukubaliana chama hicho kupewa wabunge katika Uchaguzi Mkuu ujao.

Mazungumzo hayo ya maridhiano yanasimamiwa na Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe. Mwishoni mwa wiki iliyopita, Lissu, akiwa katika eneo la Kibaigwa mkoani Dodoma wakati wa ziara yake ya ujenzi wa chama, alitoa hadhari kuhusu utekelezaji wa maridhiano, akionya kuwa kuna chama kilipewa ahadi za aina hiyo katika uchaguzi uliopita.

Lissu alionya kile alichokiita "nusu mkate", ni hatari kwa ustawi wa chama, akiwataka wanachama wa chama hicho wasiwachekee viongozi wao pale wanaposhindwa kukidhi matarajio yao.

Akizungumza na Nipashe juzi kuhusu kauli hiyo, Mrema alisema kupewa wabunge siyo sehemu ya hoja zao 12 walizokubaliana katika mazungumzo yao na serikali.

"Hakuna kitu kama hicho. Suala la kupewa wabunge halimo kwenye mazungumzo ya maridhiano. Tulikuwa na mambo 12 katika maridhiano na serikali. Hilo (la kupewa wabunge) halimo," alisema.

Januari 31, mwaka huu akiwa jijini Mwanza, Mbowe alisema kuwa baadhi ya watu wamekuwa wanamtuhumu kufanya kile alichokiita "kulambishwa asali" baada ya kushiriki katika vikao vya mchakato wa maridhiano na serikali.

"Wanachama wa CHADEMA, wakiwamo viongozi wangu wakuu, ambao ninawapa haki hiyo kabisa, nao wanalalamikia usiri na kusema 'mwenyekiti kalamba asali', yaani Mbowe nilambishwe asali kuusaliti umma?" alihoji akiwa katika mkutano na wanachama na wafuasi wa chama hicho jijini Mwanza.

Katika hotuba yake ya Kibaigwa, Lissu alisema kuwa sasa yanaonekana mabango mengi mitaani, yakiwa na ujumbe kwamba mama (Rais), amemaliza uhasama kwa maridhiano, akisisitiza kuwa hapingani na suala hilo.

Hata hivyo, Lissu alisema kuwa kwa sasa kuna ahadi ambazo baadhi ya vyama viliwahi kupewa huko nyuma ikiwamo ya kupatiwa wabunge lakini haikutekelezewa.

"Ni jambo la kusikitisha kuona baadhi ya viongozi wanadai maridhiano katikati ya madai ya watu kuuawa na wengine kufunguliwa kesi kwa sababu za kisiasa. Mimi nimepigwa risasi, hakuna waliokamatwa na hatujaambiwa mpaka leo. Jiulizeni waliofunguliwa kesi ya ugaidi wameombwa msamaha?" alihoji.

Alisema kuwa maridhiano sahihi ni kuweka mfumo mzuri wa wananchi kuchagua viongozi wao katika uchaguzi huru na wa haki na mazingira hayo yasipokuwapo maridhiano hayatokuwa na maana.

"Mbowe alikuwa gaidi juzi, leo wanapiga picha ya pamoja. Je, alimwomba msamaha? Je, alisema kwanini alimwita gaidi? Na mimi nipo kwenye picha moja kubwa katikati ya njia wanasema 'mama ameleta maridhiano'," Lissu alisema.




Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot (kulia), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Alpha Mundi (AMF), Lade Araba (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Usaidizi wa biashara ndogo (SEAF) Peter Righi, wakikata utepe kuzindua mfuko wa kuwezesha wajasiriamali ujulikanao kama 'Daraja Impact Fund', nyumbani kwa balozi, Oysterbay jijini Dar es Salaam juzi, wenye lengo la kukuza biashara mbalimbali zilizopo kwenye mnyororo wa thamani kwa wajasiriamali wadogo, wanawake na vijana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BAWACHA waandamana kisa Mdee, wenzake

**Na Romana Mallya**

WANAWAKE wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kupitia baraza lao (BAWACHA), jana waliandamana kufikisha ujumbe kwa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kutaka kutimiza takwa la kuwaondoa wanawake 19 bungeni kwa kuwa hawana chama.

Katika maandamano yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, waandamanaji walibeba mabango yenye ujumbe mbalimbali.

'Tulia Acha Kukanyaga Katiba Ondoa COVID- 19 Bungeni', 'Kuwalipa COVID- 19 (Sh. bilioni 8.2) Matumizi Mabaya ya Fedha Zetu' na 'Tulia Ackson Wewe ni Mwanasheria Umetumia Katiba Gani Kuwaweka Hao COVID - 19 bungeni',ndivyo yalivyosomeka baadhi ya mabango yao.

Katibu Mkuu BAWACHA, Catherine Ruge, akizungumza na waandishi wa habari baada ya maandamano hayo yaliyoishia Ofisi Ndogo za Bunge, Dar es Salaam, alisema wanamtaka Spika kutimiza hilo.

"Tumeandamana kufikisha ujumbe wetu kwa Spika kumwambia kwamba anapaswa kutimiza takwa lake la kikatiba kuwaondoa wanawake 19 bungeni kwa kuwa hawana chama," alisema.

Wakiwa nje ya ofisi hizo baada ya maandamano hayo, Ruge wakati akijiandaa kusoma taarifa yao kuhusu suala hilo, alisema: "Ninaamini huko ndani mnatusikia tunaomba hata mlinzi aweze kupokea hii barua ya Spika," alisema.

Akisoma risala ikibeba kichwa cha habari 'Risala kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuhusu Kuwakumbatia Wanawake 19 Bungeni Ambao Hawana Chama', alisema BAWACHA inaungana na Watanzania wapenda haki ndani na nje ya nchi kupinga kuwapo kwao bungeni.

"Ninaomba niwakumbushe wananchi mnaotufuatilia. Wabunge 19 walivuliwa ubunge na Kamati Kuu ya Chama (CHADEMA) Novemba 27, 2020 baada ya kwenda kujiapisha bila ridhaa ya chama. Walikata rufani kwenye Baraza Kuu na mwaka 2022 baraza liliunga mkono uamuzi wa Kamati Kuu na kuwafukuza uanachama," alisema.

Alisema Ibara ya 71 ya Katiba iko wazi kwamba mbunge atakoma ubunge wake kama atakuwa amefukuzwa uanachama.

"Spika Tulia wewe ni mwanasheria na unafahamu kuwa una watu ndani ya Bunge ambao hawana sifa za kuwa wabunge. Ninakukumbusha ukiwa Naibu Spika wa Bunge la 11, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilimvua ubunge Sophia Simba na hatua zilichukuliwa haraka kwa kuondolewa bungeni.

"Vivyo hivyo wabunge wanane wa Chama cha Wananchi (CUF) walipovuliwa uanachama mara tu barua ilipofika mezani kwa Spika, alichukua hatua ya kuondoa wabunge hao. Kwa nini suala la hawa wanawake 19 unalifumbia macho? kuna nini nyuma ya pazia?," alihoji.

Kuhusu hoja kuwa kesi inaendelea mahakamani, alisema haina mashiko kwa kuwa hakuna zuio lolote la mahakama linalowapa kinga ya kuendelea kuwa ndani ya Bunge. Kutokana na hilo, alisema BAWACHA inamtaka mara moja kutumia mamlaka yake ya Spika kuwaondoa wanawake hao bungeni.

Alisema wanawake hao mpaka sasa wameshalipwa Sh. bilioni 8.2 na kueleza kuwa, hayo ni matumizi mabaya ya kodi za watanzania kwa kuwa zingeweza kujenga vituo vya afya 20 au shule 40 za msingi au ofisi 40 za walimu.

Pia alisema BAWACHA inatoa rai kwa Watanzania kuendelea kupinga kitendo cha Spika kuendelea kutumia kodi zao kwa kulipa watu waliowaita hawastahili.

# BOCCO AFUNGUKA SIMBA ITAREJEA KIBABE 2023/24

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa Simba, John Bocco amewaomba wanachama na mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi kushuhudia mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam huku akiahidi msimu ujao kikosi cha Wekundu wa Msimbazi kitarejea na nguvu kubwa.

**Kauli hiyo imetokana na Simba kuondolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na michuano ya Kombe la FA, hivyo kumaliza msimu bila kikombe chochote.**

Akizungumza na Nipashe jana, Bocco, alisema yaliyotokea ni mambo ya soka, akiahidi kuwa viongozi wao watakikifanyia marekebisho kikosi na msimu ujao watarejea na nguvu mpya, huku akiwataka leo kwenda kuishangilia timu hiyo Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salam, watakaposhuka dhidi ya Ruvu Shooting.

Bocco alisema kadhia ya kuzomewa na mashabiki walipokuwa wanarejea kutoka Mtwara, iliwaumiza pia wachezaji kwa sababu wameshindwa kuwapoza mashabiki na kufikia malengo.

"Kwanza tunawashukuru sana mashabiki wetu na tuwape pole kwa sababu yale malengo tuliyojipangia sisi kama klabu, sisi wachezaji kwa asilimia kubwa hatujafanikisha, niwape pole kwa sababu wamekuwa wanatupa sapoti sana na walitegemea tutafanya vyema msimu huu, lakini haikuwa hivyo, mimi kama nahodha kwa niaba ya wachezaji wenzangu wanapa pole, na wanapongeza kwa sapoti wanayotupa siku zote na tangu kuanza kwa msimu huu," Bocco alisema.

Mshambuliaji huyo amewataka wanachama na mashabiki wao kutokata tamaa na badala yake waendelee kuiamini timu yao.

"Tunaomba wasikate tamaa waendelee kuiamini timu yao, naamini kabisa tuna viongozi thabiti na wameona mapungufu katika ikosi chetu, na wameona nini ambacho wanatakiwa kurekebisha kwa msimu ujao.

Naamini msimu ujao tutarudi kwa nguvu zaidi, Mungu akisaidia tunaweza kufikia malengo, tunaomba tu mashabiki waendelee kusapoti timu, hizi ni nyakati za mpito, kama mwanzo tulipokuwa tunashinda, basi sasa hivi tumepoteza, tutainuka na kusonga mbele," alisema Bocco.

Kuelekea mechi dhidi ya Ruvu Shooting inayoburuza mkia mpaka sasa ikiwa na pointi 20, nyota huyo alisema wamejiandaa kusaka matokeo bora ili kumaliza msimu na heshima.

"Tangu tupoteze mchezo wetu wa nusu fainali ya Kombe la FA, mazoezi yanaendelea, tumeshapoteza vikombe vyote tulivyokuwa tunapigania, lakini ni nafasi kubwa kwa sisi wachezaji kutumia hizi mechi kama kuwatia moyo mashabiki wetu na kumaliza msimu huu vizuri katika mechi tatu zilizobakia, hivyo tunaomba mjitokeze kwa ajili ya kutuunga mkono," nahodha huyo aliwasihi Wanasimba.




Waogeleaji wenye umri kuanzia miaka tisa wa klabu ya FK Blue Marlins ambao wanajiandaa kushiriki mashindano mbalimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kidunda, Mukadi ulingoni Juni

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa kutoka Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Selemani Kidunda, anatarajia kupigana na Mkongomani Eric Mukadi katika pambano litakalofanyika Juni 30, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.


Tayari Kidunda ameingia mkataba na waandaaji wa pambano hilo na Kampuni ya PAF Promotion Entertainment.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Fadhili Maogola, alisema wameamua kumchukua Kidunda katika pambano hilo kutokana na kutambua ubora wake. Maogola alisema mpinzani wa Kidunda anaishi Afrika Kusini na alitaja pambano lingine litakuwa ni kati ya Mfaume Mfaume dhidi ya Nkululeko Mhlongo, raia wa Afrika Kusini.

"Pambano letu 'La hata usipo lala patakucha', yeye (Kidunda) na Mfaume watapanda katika ulingo mmoja siku hiyo pale Mlimani City ili kuonyesha ukali wao, hakuna asiyejua ubora na wake," alisema Maogola.

Naye Kidunda alisema anashukuru kwa kupata pambano hilo kwa sababu mara ya mwisho alipanda ulingoni Songea mwaka jana dhidi ya Mkongomani mwingine, Katompa.

"Nataka kuwaambia mashabiki zangu narudi tena kwa moto mkubwa maana siku zote mimi sipigani ila nacheza ngumi."




Kidunda

## Klabu 13 kuchuana FK Blue Marlins

**Na Saada Akida**

KLABU 13 zitashiriki katika mashindano ya kwanza ya kuogelea ya FK Blue Marlins yaliyopangwa kuanzia kesho kwenye bwawa la kuogelea la Shule ya Kimataifa ya FK ya Bahari Beach.

Klabu hizo ni Dar Swim Club, Bluefins, Taliss-IST, Lake Swim Club, Champion Rise, Wahoo Zanzibar, Braeburn Sharks, Pigec, Majimaji, Mis Piranhas, Premier Swim, Train To Gain na wenyeji FK Blue Marlins.

Meneja wa klabu ya FK Blue Marlins, Opalina Nanyaro, alisema jana waogeleaji 232 watashindana katika mashindano hayo ambayo yatamalizika Jumapili.

Opalina alisema zawadi na medali mbalimbali zitatolewa kwa washindi waogeleaji watatu bora huku pia medali zitatolewa kwa timu zitakazoshinda katika mashindano ya relei.

Aliongeza waogeleaji watashindana katika umri tofauti katika staili mbalimbali ikiwamo Individual Medley (IM), butterfly, backstroke, breaststroke na freestyle.

## Coastal Union SC yakomaa na Ihefu Bara

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Coastal Union kimeingia kambini kujiandaa na mechi dhidi ya Ihefu itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini, Tanga huku kikitamba mchezo huo utakuwa sawa na fainali.



Kocha Mkuu wa Coastal Union, Fikirini Elius (pichani), amesema watafanya kila juhudi kuhakikisha wanashinda mechi hiyo ingawa wanajua itakuwa ngumu lakini wao wanataka kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kubakia katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Ni mchezo wa aina yake, Ihefu wana timu nzuri, lakini hata sisi tuna timu nzuri tu, tunapishana mambo madogo madogo tu," alisema Elius.

Naye mchezaji, Jackson Shiga, aliliambia gazeti hili ingawa wamebakisha mechi tatu ili wamalize msimu huu, lakini mechi ya dhidi ya Ihefu inawaumiza kichwa na wao kama wachezaji wameahidi kupambana kusaka ushindi.

Coastal Union ipo katika nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 30 mkononi.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### LLORIS ANUKIA SAUDIA

KIPA wa wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Hugo Lloris, mwenye umri wa miaka 36 ana ofa ya kucheza Saudi Arabia msimu ujao kwa mshahara ambao ni mara tatu ya ule anaopokea sasa katika timu hiyo ya Ligi Kuu England. ***(Times)***

#### MADDISON NA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle imefufua nia yao ya kumnunua kiungo wa Leicester mwenye umri wa miaka 26, James Maddison. ***(Telegraph)***

#### TCHOUAMENI KUTUA LIVER

LIVERPOOL imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Aurelien Tchouameni, mwenye umri wa miaka 23, walau kwa mkataba wa mkopo. ***(90 Min)***

#### SPURS IKO MAWINDONI

KLABU ya Tottenham Hotspur inamtafuta atakayechukua nafasi ya mkurugenzi mkuu wa zamani, Fabio Paratici kabla ya kukamilisha mipango ya kumsajili kocha mpya. ***(Mirror)***

#### CITY YAMFUATILIA MATEO

KLABU ya Manchester City imeelekeza darubini yao kwa kiungo wa kati wa Chelsea na Croatia, Mateo Kovacic, 29, kama mbadala wa kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham (19), ambaye anatazamiwa kujiunga na Real Madrid kutoka Borussia Dortmund. ***(Football Insider)***

#### ZIELER ATAJWA LIVERPOOL

KLABU ya Liverpool iko tayari kumsajili mchezaji wa zamani wa timu ya taifa ya Ujerumani na Hannover 96, Ron-Robert Zieler, 34, kama kipa wa ziada. ***(Bild)***

#### OSIMHEN THAMANI JUU

NAPOLI imeongeza bei ya nyota wake, Victor Osimhen, hadi kufikia euro milioni 160 wakitarajia kinyang'anyiro kikali baina ya klabu zinazomwania mshambuliaji huyo wa Nigeria mwenye umri wa miaka 24. ***(Il Matino)***

#### LEAO ASAINI MITANO

MSHAMBULIAJI wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Ureno, Rafael Leao mwenye miaka 23, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool na Chelsea, amesaini mkataba mpya wa miaka mitano na klabu hiyo ya Italia. ***(Athletic)***

#### MARTINEZ ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United inamfuatilia mshambuliaji wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Argentina, Lautaro Martinez, 25. ***(Football Insider)***

#### RAMSDALE KIMEELEWEKA

KIPA, Aaron Ramsdale, 24, anakaribia kuafiki mkataba mpya wa muda mrefu na Arsenal. ***(ESPN)***

#### SUNDERLAND NA CLARKE

KLABU ya Sunderland inapanga kumpa mkataba mpya, Jack Clarke, 22, ili kusambaratisha nia ya Crystal Palace na Brentford kumnunua mshambuliaji huyo. ***(TeamTalk)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BUSQUETS RASMI KUONDOKA BARCA

**BARCELONA,** Hispania

●●● Kiungo huyo asema amepitia wakati mgumu kufanya uamuzi huo...

NYOTA wa Barcelona, Sergio Busquets ametangaza ataondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu baada ya miaka 18 akiwa Camp Nou.

**Kiungo huyo wa kati wa Hispania alijiunga na timu hiyo ya Katalunya akiwa chipukizi mwaka 2005 na amecheza mechi 719 kwenye kikosi cha kwanza.**

Katika taarifa iliyoko kwenye tovuti ya Blaugrana, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 alisema: "Imekuwa heshima na fahari kuvaa beji hii lakini kila kitu lazima kifikie mwisho.

"Haujakuwa uamuzi rahisi lakini wakati umefika."

Kitendo cha mwisho cha Busquets katika klabu hiyo kinatarajiwa kunyanyua taji lake la tisa la LaLiga, huku Barca kwa sasa wakiwa na pointi 13 na wamesaliwa na mechi tano. Gwiji wa kweli wa wababe hao wa LaLiga, Busquets pia alikuwa kitovu cha ushindi wa tatu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya

Aliunda ushirikiano wa kipekee wa safu ya kati na bosi wa sasa, Xavi na Andres Iniesta, huku watatu hao wakiimarika hasa wakati wa utawala wa, Pep Guardiola pale Katalunya.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania alikabidhiwa unahodha baada ya kuondoka kwa, Lionel Messi mwaka 2021 na amecheza mechi 39 katika mashindano yote msimu huu.

Ripoti za awali zinaonyesha huenda akahamia Saudi Arabia au Ligi Kuu ya Marekani (MLS).

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,112,46

MECHI KALI
SIMBA
VERSUS
RUVU SHOOTING
1 | 1.03
X | 7.17
2 | 25.47

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# INZAGHI: INTER HAIJAMALIZA KIBARUA

**MILAN,** Italia

KOCHA, Simone Inzaghi, amesisitiza Inter bado wana kazi ya kufanya ili kutinga hatua ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ushindi wa mabao 2-0 walioupata katika mkondo wa kwanza dhidi ya AC Milan hapo juzi.

Inter waliwafunga wapinzani wao wa jiji dakika 11 za kwanza kupitia kwa Edin Dzeko na Henrikh Mkhitaryan na kuuweka mchezo huo mikononi mwao kwa urahisi katika kipindi cha kwanza.

Milan waliimarika baada ya mapumziko lakini watashukuru bado wanaweza kuwafikia mabingwa hao wa 2010 baada ya matokeo ya kutatanisha mbele ya wafuasi wao kwenye mechi ya 'nyumbani' ya sare.

Inzaghi aliiambia Amazon Prime Video: "Tungeweza kufanya zaidi ya mabao hayo mawili, lakini mechi nzuri. Tayari tumepitia raundi kadhaa, tunajua tuko mbele.

"Sasa kutakuwa na mkondo wa pili, tutakuwa na mashabiki wetu na tunajua wazi bado tutalazimika kufanya bidii ili kutimiza ndoto.

"Niliomba jana (juzi) kwa moyo na akili. Walifunika kila inchi ya uwanja na walioingia walitusaidia.

"Hivyo ndivyo maonyesho kama haya yanavyofanywa. Sasa ni sawa kuwa na furaha, lakini tunajua bado tuna kazi."

Naye mmoja wa wafungaji wa mabao, Dzeko aliwaonya wachezaji wenzake kutokata tamaa kabla ya mechi ya mkondo wa pili itakayochezwa Jumanne ijayo.

Bosi wa Milan, Stefano Piolo, alikasirishwa na mbinu ya timu yake.

Aliiambia Amazon Prime Video: "Tutajaribu kufanya vizuri zaidi katika mkondo wa pili. Nadhani walipata bora zaidi ya kukaba na mipira ya pili. Mechi ilienda vibaya kutokana na mtazamo wa kimbinu na kiakili.



# Mourinho ashangaa kutakiwa na PSG

**ROME,** Italia

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, alipuuzilia mbali uvumi unaoendelea kuhusu kuchukua nafasi ya kuiongoza klabu ya Paris Saint-Germain.

Kumekuwa uvumi kuna uwezekano wa kuchukua klabu hiyo ya Ligue 1 kutoka kwa Christophe Galtier, msimu ujao.

Lakini Mourinho alisisitiza uaminifu wake kwa Roma, ambapo ana mkataba hadi 2024.

"Ikiwa wangepiga simu, hawakunipata Mourinho aliambia S Sport Italia Jumatano.

"Nshangaa kuona n tajwa sehemu amba hatujafanya mawasili mo yoyote.

"Mimi ni koc wa AS Roma na vinginevyo."

62,859/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/05/23 | 17:00 | Aston Villa vs Tottenham Hotspur | 2.18 | 3.40 | 2.95 |
| 02. 13/05/23 | 17:00 | Southampton FC vs Fulham FC | 2.70 | 3.20 | 2.45 |
| 03. 13/05/23 | 17:30 | FC Vizela vs FC Famalicao | 2.55 | 3.05 | 2.70 |
| 04. 13/05/23 | 19:15 | Cercle Brugge vs KAA Gent | 2.65 | 3.15 | 2.24 |
| 05. 13/05/23 | 19:30 | Sunderland AFC vs Luton Town | 2.60 | 3.20 | 2.60 |
| 06. 13/05/23 | 19:30 | Villarreal CF vs Athletic Bilbao | 2.17 | 3.35 | 3.00 |
| 07. 13/05/23 | 19:45 | FC Volendam vs Sparta Rotterdam | 2.85 | 3.45 | 2.24 |
| 08. 13/05/23 | 21:30 | CA Independiente Avellaneda vs CA Tigre | 2.44 | 2.90 | 2.60 |
| 09. 14/05/23 | 00:00 | CA Banfield vs CA San Lorenzo de Almagro | 2.47 | 2.80 | 2.65 |
| 10. 14/05/23 | 13:30 | Hellas Verona vs Torino FC | 2.29 | 3.05 | 3.10 |
| 11. 14/05/23 | 14:00 | Coventry City vs Middlesbrough FC | 2.70 | 3.25 | 2.42 |
| 12. 14/05/23 | 15:00 | RC Celta de Vigo vs Valencia CF | 2.16 | 3.20 | 3.20 |
| 13. 14/05/23 | 16:30 | VfB Stuttgart vs Bayer Leverkusen | 2.60 | 3.40 | 2.43 |
| 14. 14/05/23 | 17:30 | Rio Ave FC vs Vitoria SC Guimaraes | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 15. 14/05/23 | 18:05 | AS Monaco vs Lille OSC | 2.60 | 3.50 | 2.37 |
| 16. 14/05/23 | 19:00 | Bologna FC vs AS Roma | 3.15 | 3.00 | 2.28 |
| 17. 14/05/23 | 20:00 | Defensa y Justicia vs Estudiantes de La Plata | 2.26 | 2.85 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 12/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 2285 | KMC vs Singida BS FC | 2.50 | 2.84 | 2.79 |
| 16:00 | 5192 | Napsa Stars vs Forest Rangers | 1.75 | 3.44 | 4.06 |
| 17:00 | 5327 | Qizilqum vs FC Olimpik | 2.47 | 2.89 | 2.78 |
| 17:15 | 3688 | Al Ain vs AL Bataeh (UAE) | 1.16 | 6.40 | 11.35 |
| 17:15 | 4563 | Dibba Al Fujairah vs Al Dhafra | 1.33 | 4.62 | 6.97 |
| 17:30 | 3834 | Voluntari vs Botosani | 2.01 | 3.09 | 3.72 |
| 18:00 | 4355 | Sandnes Ulf vs Kristiansund | 3.08 | 3.54 | 1.99 |
| 18:00 | 4625 | Zira vs Kapaz | 1.72 | 3.47 | 4.35 |
| 18:00 | 4893 | FK Sloga Doboj vs Zrinjski Mostar | 7.47 | 4.46 | 1.35 |
| 19:00 | 1685 | Velez Mostar vs FK Igman Konjic | 1.56 | 3.57 | 5.58 |
| 19:00 | 3819 | GKS Piast Gliwice vs Korona Kielce | 1.68 | 3.39 | 4.52 |
| 19:00 | 4106 | Simba vs Ruvu Shooting | 1.03 | 7.17 | 25.47 |
| 19:00 | 5388 | Slaven Belupo vs Lokomotiva Zagreb | 2.68 | 3.09 | 2.42 |
| 19:30 | 1228 | Sandhausen vs Hansa | 2.77 | 3.22 | 2.45 |
| 19:30 | 3765 | Magdeburg vs Nurnberg | 2.17 | 3.59 | 2.93 |
| 20:00 | 3256 | Odd Ballklubb vs Lillestrom | 2.72 | 3.30 | 2.41 |
| 20:00 | 3837 | CD Trofense vs CF Estrela | 2.87 | 3.29 | 2.26 |
| 20:00 | 5608 | Jonkopings Sodra vs AFC Eskilstuna | 1.95 | 3.46 | 3.73 |
| 20:30 | 1690 | WSG Wattens vs Josko Ried | 2.02 | 3.33 | 3.18 |
| 20:30 | 5557 | Rapid Bucuresti vs Sepsi Osk | 2.12 | 3.24 | 3.24 |
| 21:00 | 1246 | PEC Zwolle vs Roda Kerkrade | 1.28 | 5.38 | 7.66 |
| 21:00 | 1683 | FC Eindhoven vs Helmond Sport | 1.50 | 4.07 | 5.43 |
| 21:00 | 1856 | Twente vs NEC Nijmegen | 1.45 | 4.40 | 5.80 |
| 21:00 | 3055 | Maastricht vs Telstar | 2.45 | 3.38 | 2.56 |
| 21:00 | 3179 | Jong Ajax vs Jong AZ Alkmaar | 2.09 | 3.65 | 2.92 |
| 21:00 | 3545 | NAC Breda vs Heracles Almelo | 3.38 | 3.64 | 1.91 |
| 21:00 | 3582 | Den Bosch vs Almere City | 4.81 | 4.08 | 1.56 |
| 21:00 | 3651 | Willem II Tilburg vs Jong Utrecht | 1.20 | 6.02 | 10.17 |
| 21:00 | 3952 | Sport Huancayo vs UTC Cajamarca | 1.58 | 3.64 | 4.93 |
| 21:00 | 5421 | VVV Venlo vs De Graafschap | 2.77 | 3.60 | 2.19 |
| 21:00 | 5802 | FC Oss vs Jong PSV | 2.81 | 3.48 | 2.21 |
| 21:00 | 5870 | ADO Den Haag vs Dordrecht | 1.44 | 4.38 | 5.84 |
| 21:15 | 1418 | Lausanne-Sport vs Neuchatel Xamax | 1.42 | 4.21 | 5.96 |
| 21:30 | 1609 | FC Koln vs Hertha BSC | 1.79 | 3.61 | 3.91 |
| 21:30 | 2329 | Legia Warszawa vs Jagiellonia | 1.58 | 3.75 | 4.73 |
| 21:45 | 1852 | Bohemians FC vs Derry City | 2.78 | 3.09 | 2.34 |
| 21:45 | 2525 | Queens Park vs Partick Thisle | 2.63 | 3.42 | 2.43 |
| 21:45 | 2786 | Dundalk FC vs Cork City | 1.84 | 3.34 | 3.75 |
| 21:45 | 4317 | St Patricks vs Drogheda Utd | 1.76 | 3.49 | 3.90 |
| 21:45 | 4943 | Galway United vs Wexford Youths | 1.21 | 5.35 | 10.08 |
| 21:45 | 4960 | Clyde vs East Fife | 1.92 | 3.44 | 3.54 |
| 21:45 | 5132 | UCD Dublin vs Shamrock Rovers | 10.27 | 5.55 | 1.20 |
| 21:45 | 5759 | Lazio vs Lecce | 1.65 | 3.44 | 5.19 |
| 22:00 | 3013 | Esperance Tunis vs Al Ahly Cairo | 2.29 | 2.79 | 3.18 |
| 22:00 | 4322 | Lens vs Reims | 1.53 | 4.12 | 5.22 |
| 22:00 | 5036 | Peterborough vs Sheffield Wed | 2.62 | 3.23 | 2.57 |
| 22:00 | 5490 | Mallorca vs Cadiz CF | 2.07 | 2.91 | 3.81 |
| 22:00 | 5722 | Burgos vs Leganes | 2.31 | 2.95 | 3.15 |
| 22:15 | 4722 | Gil Vicente vs Boavista | 2.16 | 3.32 | 3.12 |
| 23:30 | 2243 | FBC Melgar vs Sport Boys Association | 1.26 | 4.73 | 9.26 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# RAGE AWAOMBA SIMBA KUISHANGILIA YANGA CAF

**Na Hadija Mngwai**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Simba, Ismail Aden Rage, amewataka Watanzania wote ikiwamo mashabiki wa klabu yake kuungana pamoja kuiombea Yanga ili itinge fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika wanayoshiriki.

Yanga imeweka mguu mmoja ndani katika hatua ya fainali baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 katika mechi yake ya kwanza ya nusu fainali dhidi ya Marumo Gallants kutoka Afrika Kusini iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

**Timu hizo zitarudiana wiki ijayo huko Johannesburg, Afrika Kusini.**

Akizungumza na Nipashe jana, Rage, alisema ushindi walioupata Yanga ni mzuri na unawafanya waende kucheza kwa kujilinda katika mchezo wa marudiano na hatimaye kusonga mbele katika michuano hiyo.

Rage alisema kwa sasa Yanga inapeperusha bendera ya Tanzania, hivyo ni wajibu wa kila shabiki kuungana nao kwenye hatua waliyofikia.

"Kipindi cha kwanza Yanga walitoa nafasi kwa wapinzani ambazo hawakuweza kuzitumia lakini kipindi cha pili walifanya vizuri na kushinda.

" Huu ni ushindi mzuri sana ambao Yanga wameupata, wakienda South (Afrika Kusini), watakwenda kucheza mpira wa kujilinda muda wote, wana nafasi kubwa ya kwenda hatua ya fainali, hivyo nawatakia kila la kheri.

Naomba Watanzania wote tuweke pembeni tofauti zetu na tuiombee Yanga ifike fainali kwa sababu inaiwakilisha Tanzania," alisema Rage.

## Simba yaitangazia 'ubaya' Ruvu

INATOKA UK. 23

ya leo wanaenda kuangalia namna ya kujiondoa mkiani na kurejesha matumaini ya kuibakiza timu katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tumejiandaa vizuri na mikakati yetu ni kuona jinsi gani tunashinda mchezo huu ili kuondoka hapa chini, kama tunaweza kuinusuru timu," alisema Msese.

Katika maandalizi mengine kuendelea mechi dhidi ya Singida Big Stars itakayochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Kocha Msaidizi wa KMC, Adam Khalid, alisema maandalizi yao yako vizuri na wanaamini watazibakisha pointi zote tatu ili kujinusuru na janga la kushuka daraja.

"Tumejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo wetu dhidi ya Singida Big Stars kupata matokeo bora, hatuna majeraha yeyote na tunaingia kwa tahadhari kubwa kwa sababu tunatakiwa kujiondoa katika hatari zaidi," alisema Khalid.

Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, alisema watashuka dimbani kwa tahadhari kwa ajili ya kutafuta ushindi dhidi ya wapinzani wao.

"Mechi haitakuwa rahisi kwa sababu ukiangalia wapinzani wetu wako katika nafasi mbaya, na sisi tunahitaji kupata matokeo mazuri katika mchezo huo ili kuendelea kubakia kwenye nafasi ya tatu," alisema Pluijm.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Asha Djafar (kushoto), akijiandaa kuwatoka wachezaji wa Baobab Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma juzi. Simba Queens ilishinda mabao 2-0. **PICHA: SIMBA SC**

## *Serikali yaipongeza Yanga*

INATOKA UKURASA 24

huku kipindi cha pili Yanga ikipata nafasi ya kutawala mchezo na kutumia mapungufu yaliyopelekea kuondoka na ushindi.

"Nimeumizwa zaidi na bao la pili la Yanga, kwa safu ya ulinzi kufanya makosa yaliyotugharimu, lakini tunaenda kufanyia kazi na mechi haijaisha, bado dakika 90 za marudiano zitakazikuwa nyumbani," alisema Kerr.

Yanga inahitaji sare au ushindi wowote ili kutinga fainali ya mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Kabla ya mechi hiyo ya marudiano, Yanga itakutana na Dodoma Jiji FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara na endapo itashinda, itatangwa mabingwa wapya wa msimu huu huku wakibakiwa na mechi mbili za mkononi.

# Michezo

Ijumaa Mei 12, 2023

Nipashe




Busquets rasmi kuondoka Barca

UKURASA 21

# Serikali yaipongeza Yanga SC

## ●●● Majaliwa awaambia Watanzania wanaitaka fainali CAF, Nabi acharuka...

**Saada Akida na Augusta Njoji,**

DODOMA

WAKATI Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipongeza Yanga kwa ushindi wa mabao 2-0 walioupata katika mechi ya kwanza ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nassredine Nabi, amesema hajaridhishwa na namna kiwango kilichoonyeshwa na nyota wake.

**Yanga itawafuata Marumo Gallants kwa ajili ya mechi ya marudiano itakayochezwa Mei 17, mwaka huu nchini Afrika Kusini.**

Akizungumza bungeni jana, Majaliwa, alisema klabu hiyo imeendelea kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika mashindano hayo ya kimataifa.

“Tunawaombea sana katika mchezo wa marudiano kule Afrika Kusini mshinde kwa magoli mengi, Watanzania wana hamu ya kuona Tanzania inaingia katika mashindano haya ngazi ya fainali,” Majaliwa alisema.

Aidha, aliipongeza Simba kwa hatua iliyofikia na anaamini wamejifunza na kuona kutoka kwa majirani zao.



“Tunaamini msimu ujao vilabu vyetu viwili au zaidi vitafanya vizuri sana,” alisema kiongozi huyo.

Nabi aliiambia Nipashe baada ya mechi kumalizika, wachezaji wake hawakucheza kama alivyowaelekeza katika uwanja wa mazoezi hasa katika kipindi cha kwanza cha mechi hiyo.

Nabi alisema walishindwa kutumia nafasi walizotengeneza katika kipindi cha kwanza kama alivyotarajia kupata ushindi mnono kwenye mechi ya uwanja wa nyumbani.

“Hatukucheza vizuri kama tulivyotarajia, tulifanya mazoezi vyema na kuiandaa mbinu tuliyoanza nayo leo (juzi), lakini wachezaji walishindwa kufanya kama tulivyowafundisha na kuwaelekeza mazoezini.

Pamoja na yote tunashukuru kwa ushindi na sasa tunarudi kujipanga kwa ajili ya mechi ya maruduano tunayoamini itakuwa ngumu ugenini ila tunahitaji matokeo yatakayotufanya kutinga fainali,” alisema Nabi.

Kocha huyo aliongeza wachezaji wake walishindwa kufanya maamuzi ya haraka kwa wakati na usahihi katika dakika 45 za kwanza na kupelekea kuonyesha mchezo ambao hakuufurahia.

“Wao (Marumo Gallants) ni wazuri sana katika kukaa na mpira na kutengeneza nafasi ambazo wameshindwa kuzitumia lakini pamoja na hivyo si wazuri sana katika kujilinda . Nasikitika kuona hatukuwa katika wakati wetu mzuri, muhimu ni ushindi tunafurahi, lakini yatutaka kusubiri mechi ya marudiano, kazi bado, kazi iendelee,” alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Marumo Gallants, Dylan Kerr, alilalamika safu yake ya ushambuliaji ilishindwa kutumia vyema nafasi walizotengeneza katika kipindi cha kwanza.

Kerr, kocha wa zamani wa Simba, alisema walitengeneza nafasi lakini washambuliaji wake hawakuwa makini katika kumalizia

INAENDELEA UKURASA 23



Mshambuliaji wa Yanga, Stephanie Aziz Ki, akishangilia baada ya kufunga bao la kwanza katika mechi ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yaitangazia ‘ubaya’ Ruvu

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutofikia malengo iliyojiwekea msimu huu, Simba imeweka wazi hawatamaliza msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara kinyonge kutokana na kujipanga kuvuna pointi zote tisa katika michezo mitatu iliyobakia, imeelezwa.

Simba leo inawakaribisha Ruvu Shooting katika mechi ya raundi ya 28 ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera ‘Robertinho’ alisema maandalizi yako vizuri na malengo yake ni kumaliza ligi kwa kupata matokeo chanya kuanzia mechi yao ya leo.

Robertinho alisema amewaandaa wachezaji wake kuingia katika mechi hiyo kwa ajili ya kusaka ushindi huku wakitambua nafasi ambayo wapinzani wao walipo.

“Wachezaji wako tayari kwa mchezo huo na tunahitaji ushindi, haitakuwa mechi rahisi lakini tumejiandaa kupata matokeo mazuri, nimepoteza wachezaji wengi kwa ajili ya majeraha,” alisema Roboertinho.

Kocha huyo alisema anataka kuona kila mchezaji anaonyesha kiwango cha juu kwa sababu benchi lake la ufundi linaendelea na kuandaa tathminini ya kikosi cha msimu ujao.

Naye Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting, Frank Msese, alisema wako tayari kuwakabili Simba na wanajua mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu timu yao iko kwenye nafasi ya chini.

Msese alisema mechi

INAENDELEA UKURASA 23


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042